**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU CHETI DARAJA LA A (GATCE) 2020

610 UALIMU

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA UALIMU CHETI DARAJA LA A (GATCE) 2020

# 610 UALIMU

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2020**

Haki zote zimehifadhiwa.

**YALIYOMO**

DIBAJI .................................................................................................... iv

1.0 UTANGULIZI ............................................................................................ 1

2.0 TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI ....... 2

2.1 Sehemu A: Maswali ya Majibu Mafupi ........................................................ 2

2.1.1. Swali la 1: Saikolojia ................................................................................ 2

2.1.2. Swali la 2: Makuzi na Ukuaji wa Mtoto ................................................... 5

2.1.3. Swali la 3: Ushauri na Unasihi .................................................................. 7

2.1.4. Swali la 4: Nadharia za Kujifunza ............................................................ 9

2.1.5. Swali la 5: Matayarisho ya Ufundishaji ................................................... 12

2.1.6. Swali la 6: Upimaji katika Elimu ............................................................. 15

2.1.7. Swali la 7: Tathmini katika Elimu ........................................................... 17

2.1.8. Swali la 8: Elimu Jumuishi ...................................................................... 19

2.1.9. Swali la 9: Maendeleo ya Elimu Tanzania .............................................. 21

2.1.10.Swali la 10: Elimu Jumuishi .................................................................... 24

2.2 SEHEMU B: Saikolojia ya Elimu ................................................................ 26

2.2.1. Swali la 11: Nadharia za Kujifunza ......................................................... 26

2.2.2. Swali la 12: Makuzi na Ukuaji wa Mtoto ................................................. 30

2.3 SEHEMU C: Mitaala na Ufundishaji ........................................................... 34

2.3.1 Swali la 13: Ufundishaji ........................................................................... 34

2.3.2 Swali la 14: Maendeleo ya Elimu Tanzania ............................................. 38

2.4 SEHEMU D: Utafiti wa Kielimu, Upimaji na Tathmini ............................... 43

2.4.1 Swali 1a 15: Upimaji katika Elimu ........................................................... 43

2.4.2 Swali la 16: Upimaji katika Elimu ............................................................ 48

2.5 SEHEMU E: Misingi ya Elimu .................................................................... 52

2.5.1 Swali 1a 17: Uongozi wa Elimu ............................................................... 52

2.5.2 Swali 1a 18: Elimu ya Watu Wazima ....................................................... 57

3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA ........................................................................................ 61

4.0 HITIMISHO ............................................................................................... 61

5.0 MAPENDEKEZO ....................................................................................... 62

*Kiambatisho* ................................................................................................. 64

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kutoa taarifa juu ya tathmini ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika somo la Ualimu Daraja la IIIA mwaka 2020.

Taarifa hii inatoa mrejesho kwa wadau wa elimu, kama vile wanachuo, wakufunzi, wazazi, Taasisi ya Elimu Tanzania, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo inahusika na utengenezaji wa Sera ya Elimu, wadau wa maendeleo ya elimu na umma kwa ujumla kuhusu kiwango cha ufaulu cha watahiniwa. Mtihani huu ni tathmini ya mwisho inayoonesha kufanikiwa au kutofanikiwa kwa malengo ya elimu baada ya mafunzo ya kozi ya miaka miwili ya walimu tarajali wa shule za msingi.

Uchambuzi unaowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kuonesha sababu za watahiniwa kufanya vizuri, wastani au kufanya vibaya katika mtihani husika. Taarifa hii imeeleza baadhi ya sababu zilizowafanya watahiniwa wengi waweze kufanya vizuri katika mtihani huo ama kutofanya vizuri, kama vile kushindwa kutambua mahitaji ya swali, kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusiana na mada husika, kuchanganya dhana tofauti wakati wa kujibu maswali, kushindwa kutambua namna ya kujibu maswali kulingana na vitenzi vilivyotumika kuuliza swali pamoja na kukosa maarifa ya kuandika insha kwa usahihi.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika maswali waliyojibu unatoa picha halisi ya mafanikio na changamoto zinazojitokeza katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Ualimu katika vyuo vya ualimu Tanzania.

Baraza la Mitihani la Tanzania linaamini kwamba taarifa hii itawasaidia wadau wa elimu, katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji katika vyuo vya ualimu na pia katika kufadhili mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Aidha, Baraza la Mitihani linapenda kuwashukuru maafisa mitihani, wakufunzi na wadau wote waliohusika katika uchambuzi wa takwimu na utayarishaji wa taarifa hii.

Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii imeandaliwa ili kuwasilisha taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa wa mtihani wa somo la Ualimu ngazi ya cheti uliofanyika Julai 2020. Maswali ya mtihani yalitungwa kwa kuzingatia Muhtasari wa mwaka 2009 wa somo la Ualimu Ngazi ya Cheti Elimu ya Msingi.

Kwa ujumla kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika somo la Ualimu kwa mwaka 2020 kilikuwa kizuri kwani asilimia 99.55 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walifaulu.

Mtihani wa somo la Ualimu uligawanyika katika sehemu A, B, C, D na E. Sehemu A ilikuwa na maswali kumi (10) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote, kila swali lilikuwa na alama nne (4). Sehemu B (Saikolojia ya Elimu), C (Mitaala na Ufundishaji), D (Utafiti wa Kielimu, Upimaji na Tathmini) na E (Misingi ya Elimu) zilikuwa na maswali mawili (2) kila moja, na mtahiniwa alitakiwa kujibu swali moja tu kutoka kila sehemu. Sehemu B, C, D na E zilikuwa na alama (15) kila moja. Hivyo mtihani ulikuwa na maswali kumi na nane (18) na mtahiniwa alitakiwa kujibu jumla ya maswali kumi na nne (14).

Ufaulu wa watahiniwa umegawanywa katika viwango vitatu ambavyo ni 'ufaulu mzuri, ufaulu wa wastani', na 'ufaulu hafifu'. Ufaulu wa kiwango kizuri unaanzia alama 70 hadi 100; kiwango cha wastani alama 40 hadi 69; na kiwango hafifu alama 0 hadi 39. Aidha, kiwango cha ufaulu kwa kila swali katika sehemu A kitakuwa *kizuri* ikiwa mtahiniwa atapata alama kuanzia 3 hadi 4, kiwango cha *wastani* kuanzia alama 2 hadi 2.5 na kiwango *hafifu* kuanzia alama 0 hadi 1.5. Kwa maswali ya sehemu B, C, D na E, kiwango cha ufaulu katika kila swali kitakuwa *kizuri* ikiwa mtahiniwa atapata alama kuanzia 10.5 hadi 15, kiwango cha *wastani* kuanzia alama 6 hadi 10 na kiwango *hafifu* kuanzia alama 0 hadi 5.5.

Katika kufanya uchambuzi na kutafsiri ufaulu wa watahiniwa, aina tatu za rangi zimetumika katika chati, grafu na majedwali ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu wa kiwango kizuri, rangi ya njano inawakilisha ufaulu wa kiwango cha wastani na rangi nyekundu inawakilisha ufaulu wa kiwango hafifu.

Taarifa hii inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa kila swali na kila mada. Pia baadhi ya sampuli za majibu ya watahiniwa waliofanya swali vizuri au vibaya

zimeambatishwa kwa lengo la kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Ualimu.

# 2.0 TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

## 2.1 Sehemu A: Maswali ya Majibu Mafupi

Sehemu A ilikuwa na maswali kumi (10) yaliyolenga kuwapima watahiniwa maarifa waliyoyapata kwa kipindi cha miaka miwili (2) katika somo la Ualimu katika mada zifuatazo: *Matayarisho ya Ufundishaji, Ushauri na Unasihi, Uongozi wa Elimu Tanzania, Elimu Jumuishi, Nadharia za Kujifunza, Tathmini katika Elimu, Elimu ya Watu Wazima, Ufundishaji, Upimaji katika Elimu, Maendeleo ya Elimu Tanzania, Makuzi na Ukuaji wa Mtoto,* na *Saikolojia*. Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama arobaini (40). Kila swali lilikuwa na alama nne (4).


### 2.1.1. Swali la 1: Saikolojia

Swali hili lililenga kuwapima watahiniwa katika dhana ya saikolojia hasa katika matawi ya saikolojia. Swali liliuliza:

*Eleza kwa kifupi kazi ya msingi ya matawi ya saikolojia yafuatayo:*
*(a) Saikolojia ya elimu ya Jamii*
*(b) Saikolojia ya makuzi*
*(c) Saikolojia ya viwanda*
*(d) Saikolojia ya unasihi*


Swali lilitoka katika mada ya "Saikolojia" kipengele cha Dhana ya Saikolojia.

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonesha kuwa kati ya watahiniwa 3,363 waliofanya swali hili, watahiniwa 2,283 (67.9%) walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu wa kupata alama kuanzia 3 hadi 4. Aidha, watahiniwa 888 (26.4%) walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu wa kupata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na watahiniwa 192 (5.7%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu wa kupata alama kuanzia 0 hadi 1.5. Kwa ujumla, kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa wengi (94.3%) walipata alama kuanzia 2 hadi 4. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa kwa asilimia katika swali hili.




**Chati Na. 1:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 1.*


Watahiniwa (67.9%) waliojibu swali hili vizuri walieleza kazi za msingi za matawi ya Saikolojia. Watahiniwa walieleza kuwa: Saikolojia ya elimu ya jamii ni *tawi linaloshughulikia mahusiano ya watu katika jamii*. Saikolojia ya unasihi ni *tawi linaloshughulikia na kuchunguza na kutoa tiba kwa watu wenye matatizo ya kisaikilojia*. Saikolojia ya makuzi ni *tawi linaloshughulika na ukuaji wa binadamu tangu kutungwa mimba hadi kipindi chote cha maisha. Saikolojia ya Viwanda ni tawi la saikolojia linalojishughulika na ujenzi wa mahusiano kati ya uongozi na wafanyakazi wa viwandani*. Kielelezo 1.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


1 Kueleza maana ya :-
a) Saikolojia ya elimu ya jamii
- Hii ni tawi moja wapo la saikolojia ambalo hujihusisha zaidi na mafunzo yote ya kijamii mfano Ushirika wa watu katika jamii, Mahusiano yao na kadhalika.
b) Saikolojia ya makuzi
- Hili ni tawi moja wapo la Saikolojia ambalo hujihusisha zaidi na ukuaji wa binadamu tangu kutungwa kwa mimba mpaka anapozaliwa na hata kuwa mkubwa mpaka mwisho wa maisha yake.
c) Saikolojia ya Viwanda
- Hili ni tawi moja wapo la saikolojia ambalo hihusisha zaidi na mazingira ya viwandani ~~kati~~ katika kufanya mahusiano mazuri kati ya wafanyakazi na viongozi wa kiwanda husika.
d) Saikolojia ya unasihi
- Hili ni tawi la saikolojia ambalo hujihusisha zaidi na utoaji wa ushauri na nasaha kwa watu mbalimbali wenye matatizo hata wasio na matatizo kwa lengo la kupunguza tatizo kwa muhusika. Mfano:- Msongo wa mawazo

Kielelezo Na.1.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 1.

Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha namna mtahiniwa alivyokuwa na uelewa juu ya mada ya Saikolojia hasa mada ndogo ya matawi ya Saikolojia. Mtahiniwa aliweza kueleza kwa mujibu wa mwongozo wa usahihishaji kazi za msingi za matawi ya saikolojia aliyotakiwa kueleza.

Uchambuzi wa viwango vya ufaulu wa watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa (5.7%) waliokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu hawakuwa na maarifa ya kutosha kueleza kazi za msingi za matawi ya Sakoilojia. Kielelezo Na. 1.2. ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutoa majibu sahihi katika swali hili.



1. Kueleza kwa kifupi kazi ya msingi ya matawi haya.

a) Saikolojia ya Elimu ya Jamii
kazi ya tawik hili ni
kuhakikisha Elimu inatolewa
kwa kuzingatia vigezo vyote vya Elimu

b) Saikolojia ya makuzi
kusaidia kuboresha na kuimarisha
huduma zote zinazo husika katika ma
kuzi

c) Saikolojia ya viwanda
kuhakikisha viwanda vina zalisha
malighafi ipasavyo

d) Saikolojia ya unasihi
kusaidia kusimamia masuala ya
ya unasihi na kuyapima kwa ndani

Kielelezo Na. 1.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 1.

Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza kwa ufasaha kazi za msingi za matawi ya saikolojia yaliyokuwa yametolewa. Majibu ya mtahiniwa yanadhihirisha kuwa mtahiniwa hakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu kazi za msingi za matawi ya saikolojia.

### 2.1.2. Swali la 2: Makuzi na Ukuaji wa Mtoto


Swali hili lilikusudia kuwapima watahiniwa maarifa waliyonayo kuhusu umuhimu wa mwalimu kusoma saikolojia ya makuzi ya mtoto. Swali liliuliza:

*Kwa kutumia hoja nne, bainisha umuhimu wa mwalimu kusoma saikolojia ya makuzi ya mtoto.*

Swali lilitoka katika mada ya Makuzi na Ukuaji wa Mtoto kipengele cha dhana ya makuzi ya mtoto.


Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 3,300 (98.1%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4; na watahiniwa 43 (1.3%) walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 2 hadi 2.5. Aidha watahiniwa 20 (0.6%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 1.5. Kwa ujumla kiwango cha ufaulu wa

watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa wengi (99.4%) walipata alama kuanzia 2 hadi 4. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kimeoneshwa katika Chati Na. 2.




**Chati Na. 2:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 2.*


Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa (98.1%) waliokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu waliweza kubainisha umuhimu wa mwalimu kusoma saikolojia ya makuzi ya mtoto. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na walielewa matakwa ya swali. Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.


02. i/ Humsaidia Mwalimu kutoa Mafunzo yanayolingana na makuzi ya mtoto.
ii/ Humsaidia Mwalimu kujua kama mtoto anakua kulingana na hatua zinazotarajiwa na jamii kimwili, kiakili na kitabia.
iii/ Humsaidia Mwalimu kubaini matatizo ya wanafunzi katika ujifunzaji na kupata njia/ mbinu sahihi za kutatua matatizo hayo.
iv/ Humsaidia Mwalimu kutambua ~~tabia~~ Mabadiliko yanayojitokeza katika ukuaji wa mtoto mfano Mabadiliko ya kimaumbile (kimwili) kiakili, kitabia na kimatendo.

Kielelezo Na. 2.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 2.

Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali la 2 kwa usahihi. Mtahiniwa aliweza kubainisha umuhimu wa mwalimu kusoma saikolojia ya makuzi ya mtoto.

Aidha, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa (0.6%) waliokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu walishindwa kubainisha kwa usahihi umuhimu wa mwalimu kusoma saikolojia ya makuzi ya mtoto. Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na walishindwa kuelewa namna nzuri ya kuwasilisha majibu yao. Kielelezo 2.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


2. Umuhimu wa mwalimu kusoma Saiko
lojia ya makuzi ya mtoto.
i, Inamwezesha kutatua changamoto zita
kazomkabili:
ii, Inamwezesha kati kuelewa vyema
umuhimu wa mtoto
iii, Inamwezesha kubuni njia na mbi
nu zinazoendana naye.
iv, Inamwezesha kuamua kiwango cha
akili anachotamani wanafunzi wawe
nacho.

Kielelezo Na. 2.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 2.

Kielelzo Na. 2.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kubainisha umuhimu wa mwalimu kusoma saikolojia ya makuzi ya mtoto. Mtahiniwa anaonekana kuwa na wazo juu ya umuhimu wa mwalimu kujifunza saikolojia ya makuzi ya mtoto lakini alishindwa kuwasilisha majibu yake kwa namna nzuri yenye kuleta mantiki.


### 2.1.3. Swali la 3: Ushauri na Unasihi

Swali hili lilipima maarifa waliyonayo watahiniwa kuhusu mbinu kuu nne za unasihi. Swali liliuliza:

*Orodhesha mbinu kuu nne za unasihi*


Swali hili lilitoka kwenye mada ya Ushauri na Unasihi katika mada ndogo ya aina za unasihi.

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 1,580 (47%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 1.5 na watahiniwa 1,414 (42%) walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 4. Aidha, watahiniwa 369 (11%) walikuwa na kiwango cha ufaulu cha wastani kwa kupata alama kuanzia 2 hadi 2.5. Kwa ujumla kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa wengi (53%) walipata alama kuanzia 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 3.




**Chati Na. 3:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 3.*


Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa (42.0%) waliokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu waliweza kuorodhesha mbinu nne za unasihi kwa usahihi. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na waliweza kukidhi matakwa ya swali. Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.




Kielelezo Na. 3.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 3.

Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kuorodhesha mbinu kuu nne za unasihi kwa mujibu wa mwongozo wa usahihishaji.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa (47%) waliokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu walishindwa kuorodhesha mbinu kuu nne za unasihi. Baadhi yao hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya mbinu zinazotumika katika mchakato mzima wa kunasihi. Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


03. Mbinu kuu nne za unasihi ni tano.
i) Kuwajengea uhusiano mwema
ii) Maswali dodoso.
iii) majadiliano
iv) Kushirikisha wazazi au walezi

Kielelezo Na. 3.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 3.

Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuorodhesha mbinu kuu nne za unasihi. Majibu ya mtahiniwa yanaonesha kuwa mtahiniwa huyu hakuwa na maarifa ya kutosha juu ya mbinu sahihi za unasihi. Mtahiniwa alichanganya stadi saidizi za unasihi kama vile kujenga uhusiano; stadi za mawasiliano kama vile maswali dodoso na majadiliano. Aidha mtahiniwa alitaja hoja ya kuwashirikisha wazazi au walezi ambayo haina uhusiano na swali.


### 2.1.4. Swali la 4: Nadharia za Kujifunza

Swali hili lilikuwa linapima uelewa walionao watahiniwa juu ya dhana mbalimbali za kisaikolojia. Swali liliuliza:

*Eleza kwa kifupi maana ya maneno yafuatayo ya kisaikolojia*:
*(a) Motisha*
*(b) Kichocheo*
*(c) Uhawilishaji wa mafunzo*
*(d) Kichokoo halisi*


Swali lilitoka katika mada ya Nadharia za Kujifunza katika kipengele cha motisha na vichocheo.

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa 3,363 (100%) Kati yao watahiniwa 1,405 (41.8%) walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na watahiniwa 1,010 (30%) walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 4. Aidha, watahiniwa 948 (28.2%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 1.5. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa wengi (71.8%) walipata alama kuanzia 2 hadi 4 kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 4.




**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa watahinwa katika swali la 4.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa (30.0%) waliokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu walitambua mahitaji ya swali na walikuwa na uelewa kuhusu mada ya Nadharia ya Kujifunza. Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.



04. Zifuatazo ni maana za maneno ya kisaikolojia
(a) Motisha
- Ni msukumo unaomfanya mtu atende jambo fulani ~~kama~~ kutokana na kile kinachomsukuma kutoka moyoni.
(b) Kichocheo
- Ni kitu kinachofanya mwenendo/mwenendo alionao mtu uweze kuendelea hasa katika uf ujifunzaji.
(c) Uhawilishaji hasi wa mafunzo.
- ni kitendo kinachofanya baadhi ya maarifa aliyonayo mtu kukwamisha ujifunzaji wa kitu kipya au maarifa mapya.
(d) Kichokoo halisi.
- ni aina ya kichokoo ambacho kutokea bila kujifunza.

Kielelezo Na. 4.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 4.

Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kueleza kwa kifupi maana ya maneno ya kisaikolojia yaliyokuwa yametolewa.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa (28.2%) waliokuwa na ufaulu hafifu, walishindwa kutoa maana ya maneno ya kisaikolojia yaliyokuwa yametolewa. Aidha, watahiniwa hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya maneno hayo kama yanavyotumika katika Saikolojia. Baadhi yao hawakujibu kipengele (d) *Kichokoo halisi* au kujibu kimakosa.

Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.



Kielelezo Na. 4.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 4.

Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza kwa usahihi maneno ya kisaikolojia aliyotakiwa kuyaeleza. Aidha, mtahiniwa hakuweza kutoa hoja ya nne.


### 2.1.5. Swali la 5: Matayarisho ya Ufundishaji

Swali hili liliwataka watahiniwa watumie hoja nne kuandika kwa kifupi umuhimu wa walimu kufanya matayarisho ya ufundishaji kabla ya kuingia darasani. Swali liliuliza:

*Kwa kutumia hoja nne, andika kwa kifupi umuhimu wa walimu kufanya matayarisho ya ufundishaji kabla ya kuingia darasani.*


Swali hili lilitoka katika mada ya Matayarisho ya Ufundishaji katika kipengele cha dhana ya matayarisho ya ufundishaji.

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa watahiniwa 3,348 (99.6%) waliweza kujibu swali hili vizuri kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 4. Aidha, watahiniwa 8 (0.2%) walikuwa na kiwango cha ufaulu cha wastani kwa kupata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na watahiniwa 7 (0.2%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 1.5. Matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa wengi (99.8%) walipata alama kuanzia 2 hadi 4. Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 5.




**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika swali la 5.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa, unaonesha kuwa watahiniwa (99.6%) waliokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu waliweza kueleza kwa kifupi umuhimu wa kufanya matayarisho ya ufundishaji kabla ya kuingia darasani. Kielelezo Na. 5.1. ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.



05. Kwa kutumia hoja nne, kuandika kwa ufupi umuhimu wa mwalimu kufanya matayarisho ya ufundishaji kabla ya kuingia darasani.

i) Kuna saidia mwalimu kufundisha kwa kujiamini somo lake.

ii) Kunamsaidia mwalimu kuboresha mbinu au njia anayo kwenda kuitumia kufundisha somo lake.

iii) Kuta saidia mwalimu kufikia malengo aliyojiwekea kwa muda sahihi.


Kielelezo Na. 5.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 5.

Kielelezo Na. 5 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kuandika kwa usahihi umuhimu wa mwalimu kufanya matayarisho ya ufundishaji kabla ya kuingia

darasani. Mtahiniwa anaonekana kuwa alikuwa na uelewa mzuri juu ya mada ya matayarisho ya ufundishaji hivyo kutoa majibu sahihi.

Aidha, watahiniwa (0.2%) waliokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu, baadhi yao walichanganya hoja zinazohusu kufanya matayarisho ya ufundishaji kabla ya kuingia darasani na wengine hawakuweza kuelezea vizuri hoja walizoziandika na hivyo kupata alama pungufu.

Uchambuzi zaidi unaoenesha kuwa watahiniwa (0.2%) waliokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu walishindwa kueleza angalau hoja mbili kuonesha umuhimu wa kufanya matayarisho ya ufundishaji kabla ya kuingia darasani. Watahiniwa wote waliopata alama 0 katika swali hili ni wale ambao hawakujibu swali hili. Aidha, watahiniwa wengine walitoa hoja pungufu na kati ya hizo nyingine hazikuwa sahihi hivyo kupata alama hafifu. Kielelezo Na. 5.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali la 5 kwa usahihi.


| | |
|---|---|
| 5 | Ufuatao ni umuhimu wa walimu kufanya maandalizi |
| | kabra ya kuingia darasani. |
| | i) Humfanya mwalimu kuweza kujiamini, kwa kua mwa |
| | limu ndie muwezeshaji ni lazima afanye maandal |
| | |
| | ii) Humfanya mwalimu kufundisha ili wanafunzi wawe |
| | ze kuelewa. |

Kielelezo Na. 5.2: Sampuli ya jibu lenye mapungufu katika swali la 5.

Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyepata alama hafifu kutokana na kutoa hoja pungufu na hoja moja kati ya hizo kutokuwa sahihi. Mtahiniwa aliweza kutoa hoja moja iliyo sahihi ambapo aliandika *humfanya mwalimu kuweza kujiamini* kama umuhimu wa mwalimu kufanya matayarisho ya ufundishaji kabla ya kuingia darasani. Hoja ya pili aliyoandika *"humfanya mwalimu kufundisha ili wanafunzi waweze kuelewa* haikuwa sahihi kwani sio lazima kuwa kila mwalimu anapofanya maandalizi ya ufundishaji wanafunzi humuelewa.


### 2.1.6. Swali la 6: Upimaji katika Elimu

Swali hili lilikuwa linapima uelewa wa watahiniwa juu ya vipengele vya kuzingatia wakati wa kuandaa mwongozo wa usahihishaji. Swali liliuliza:

*Eleza kwa kifupi vipengele vinne vya kuzingatia wakati wa kuandaa mwongozo wa usahihishaji.*


Swali hili lilitoka katika mada ya Upimaji katika Elimu katika mada ndogo ya utungaji wa majaribio na mitihani.

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa watahiniwa 2,297 (68.3%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 1.5. Aidha, watahiniwa 638 (19.0%) walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 2 hadi 2.5; na watahiniwa 428 (12.7%) walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 4. Kwa ujumla, kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili kilikuwa hafifu kwani watahiniwa wengi (68.3%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5 kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 6.




**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa watahiwa katika swali la 6.*

Watahiniwa (12.7%) waliokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu waliweza kueleza kwa kifupi vipengele vinne vya kuzingatia wakati wa kuandaa mwongozo wa usahihishaji. Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.




| | |
|---|---|
| 6 | (i) Jina la mtihani |
| | (ii) Sehemu ya mtihani ambazo ni A, B C D E |
| | (iii) Majibu ya kila sehemu na jumla ya |
| | alama za kila sehemu. |
| | (iv) Jumla ya alama kwa mtihani mzima. |

Kielelezo Na. 6.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 6.

Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kueleza kwa kifupi vipengele vinne vya kuzingatia wakati wa kuandaa mwongozo wa usahihishaji. Mtahiniwa anaonesha kuwa alikuwa na uelewa mzuri juu ya mada ya upimaji hasa katika Kipenegele cha utungaji wa majaribio na mitihani.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa (19.0%) waliokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu, baadhi yao walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi hivyo kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa (68.3%) waliokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu walishindwa kujibu vizuri swali. Watahiniwa hawa walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika kueleza vipengele vya kuzingatia wakati wa kuandaa mwongozo wa usahihishaji. Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza vipengele vinne vya kuzingatia wakati wa kuandaa mwongozo wa usahihishaji.



6. Vipenge vinavyo vya kuzingatia wakati wa kuandaa mwogozo wa usahihishaji:-
i. Sehemu ya kuweka alama
Hii huonesha alama ya kila mwanafunzi aliyo pata.
ii. Sehemu ya kuandi majina ya kila mwanafunzi, Hapa mwalimu hupanga kulingana na ufaulu kuanzia wakwanza hadi wa mwisho.
iii. Sehemu ya kuonesha wastani wa kila mwanafunzi. Hii hufanya mwalimu kujumlisha alama za masomo aliyofanya kabla ya mtiani uliyopo na kutafuta wastani wake.
iv. Sehemu ya kuandika kiwango cha ufaulu.

Kielelezo Na. 6.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 6.

Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza vipengele vinne vya kuzingatia wakati wa kuandaa mwongozo wa usahihishaji. Mtahiniwa alieleza namna ya kurekodi alama za wanafunzi badala ya vipengele vya kuzingatia wakati wa kuandaa mwongozo wa usahihishaji.

### 2.1.7. Swali la 7: Tathmini katika Elimu


Swali hili lililenga kupima uelewa wa watahiniwa kuhusu mambo ya kuzingatia wakati wa kufanya tathmini ya somo. Swali liliuliza:

*Orodhesha mambo manne ya msingi ya kuzingatia wakati wa kufanya tathmini ya somo lolote.*

Swali lilitoka kwenye Mada ya Tathmini katika Elimu katika mada ndogo ya utaratibu wa kufanya tathmini katika somo.


Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 1,746 (51.9%) walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 4. Aidha, watahiniwa 1,036 (30.8%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 1.5 na watahiniwa 581 (17.3%)

walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 2 hadi 2.5. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa wengi (69.2%) walipata alama kuanzia 2 hadi 4. Kiwango hiki cha ufaulu kimeoneshwa katika Chati Na. 7.




**Chati Na. 7:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 7.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa (51.9%) waliokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu waliweza kuorodhesha mambo manne ya msingi ya kuzingatia wakati wa kufanya thathmini ya somo. Watahiniwa hawa walionesha kuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya tathmini katika elimu. Kielelezo Na. 7.1 ni jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.



7 (i) Kuzingatia malengo mahususi ya somo
(ii) uwezo au ushiriki wa wanafunzi wakati wa ufundishaji.
(iii) Kupima uwezo wao kwa kutoa mazoezi kulingana na mada ambayo ilikuwa imefundishwa
(iv) Kusahihisha mazoezi ya wanafunzi na kuona kama malengo ya somo ya mefikiwa au hayakufikiwa
(v) Kuandika tathmini ya somo kama somo limefanikiwa au halikufanikiwa

Kielelezo Na. 7.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 7.

Kielelezo Na. 7.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kuorodhesha kwa usahihi mambo ya msingi ya kuzingatia wakati wa kuandaa mwongozo wa usahihishaji.

Kwa upande mwingine, watahiniwa (17.3%) waliokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu, baadhi yao waliweza kuorodhesha mambo machache yaani kati ya mawili na matatu ya kuzingatia wakati wa kufanya tathmini ya somo.

Aidha, watahiniwa (30.8%) waliokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu walishindwa kuorodhesha mambo ya msingi ya kuzingatia wakati wa kufanya tathmini ya somo. Baadhi yao walionekana kukosa maarifa ya kutosha katika mada husika na wengine walionekana kushindwa kuelewa matakwa ya swali. Kielelezo Na. 7.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali.


7/ Mambo Muhimu wakati wa Thatimini
(i) Mazoezi ya kila Siku
(ii) Majaribio ya kila mada
(iii) Majaribio ya kila Mwezi
(iv) Mitihani ya Mwisho

Kielelezo Na. 7.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 7.

Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeorodhesha njia za kupima maendeleo ya wanafunzi badala ya mambo ya msingi ya kuzingatia wakati wa kufanya tathmini ya somo.


### 2.1.8. Swali la 8: Elimu Jumuishi

Swali hili lilikusudia kupima maarifa ya watahiniwa kuhusu mambo yanayokwamisha utekelezaji wa elimu jumuishi katika shule za msingi Tanzania. Swali liliuliza:

*Taja mambo manne yanayoweza kukwamisha utekelezaji wa elimu jumuishi katika shule za msingi Tanzania.*


Swali hili lilitoka kwenye mada ya Elimu Jumuishi katika mada ndogo ya utekelezaji wa elimu jumuishi.

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 3,183 (94.6%) walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 4. Aidha, watahiniwa 111 (3.3%) walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 2 hadi 2.5; na watahiniwa 69 (2.1%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 1.5. Kwa ujumla swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwani watahiniwa wengi (97.9%) walipata alama kuanzia 2 hadi 4. Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 8.




**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 8.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa (94.6%) waliokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu waliweza kutaja mambo manne yanayoweza kukwamisha utekelezaji wa elimu jumuishi katika shule za msingi Tanzania. Hivyo watahiniwa walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada hii. Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.




8. (i) Uhaba wa wataalamu wa kufundisha wanafun
2i wenye mahitaji maalumu.
(ii) Miundombinu mibovu.
(iii) Uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzi
a hasa kwa wanafunzi wenye mahitaji maal
umu.
(iv) Mtazamo cha hasi wa jamii

Kielelezo Na. 8.1: Sampuli ya jibu sahihi katika Swali la 8.

Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kutaja mambo manne yanayoweza kukwamisha utekelezaji wa elimu jumuishi katika shule za msingi nchini Tanzania.

Watahiniwa (3.3%) waliokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu waliweza kutaja mambo manne yanayoweza kukwamisha utekelezaji wa elimu jumuishi katika shule za msingi Tanzania ambayo baadhi hayakuwa sahihi na wengine kubainisha hoja pungufu ya matakwa ya swali.

Kwa upande mwingine, watahiniwa (2.1%) waliokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu wengi wao walikosa maarifa ya kutosha katika mada husika na wengine walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali.


8 (i) Kuwepo kwa miundo mbinu inayo wezesha wanafunzi wote wenye mahitaji maalumu
(ii) Kuwepo kwa mtaala
(iii) Kuwepo kwa vifaa vinavyo tumiwa na watoto wote.
(iv) Kuwepo kwa walimu wenye taaluma ya kufundisha watoto wote.

Kielelezo Na. 8.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 8.

Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutaja mambo manne yanayoweza kukwamisha utekelezaji wa elimu jumuishi katika shule za msingi nchini Tanzania. Mtahiniwa alitaja mambo ambayo ni chanya yaani mambo wezeshi badala ya hasi yaani yale yanayokwamisha kama ambavyo swali lilimtaka.


### 2.1.9. Swali la 9: Maendeleo ya Elimu Tanzania

Swali hili lilikusudia kupima uelewa wa watahiniwa juu ya maudhui yaliyomo katika mtaala wa kufundishia katika shule za wamisionari. Swali liliuliza:

*Kwa kutumia hoja nne, fafanua maudhui yaliyomo katika mtaala wa kufundishia katika shule za wamisionari.*

Swali hili lilitoka kwenye mada ya Maendeleo ya Elimu Tanzania katika mada ndogo ya historia ya elimu Tanzania.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa watahiniwa 2,689 (80.0%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 1.5 na watahiniwa 388 (11.5%) walikuwa na kiwango cha ufaulu cha wastani kwa kupata alama kuanzia 2 hadi 2.5. Aidha, watahiniwa 285 (8.5%) walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 4. Kwa ujumla kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili kilikuwa hafifu kwani watahiniwa wengi (80.0%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5. Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 9.




**Chati Na. 9:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 9.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa (8.5%) waliokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu waliweza kufafanua maudhui yaliyomo katika mtaala wa kufundishia katika shule za wamisionari. Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kufafanua maudhui yaliyomo katika mtaala wa kufundishia katika shule za wamisionari.

9. Mtaala ni mpango unaoandaliwa kwajili ya kufundisha na kujifunza katika kutoa maarifa stadi na mwenendo ambao upo katika muhtasari wa somo, katika kipindi cha wamissionari, kumbukumba ambayo walikuwa wanajishughulisha katika mtaala wao, kwa mfano ÷ kilimo, ufugaji, stadi za kazi, Dini, kufundishwa ni baadhi ya maudhui ya mtaala endi za wamissionari ÷

Stadi za kazi, kwasababu ni ilikuwa inawasaidia katika kujikwamua kimaisha kama ushe, uhunzi, useremala, makenika.

Kilimo, ili kuweza kujipatia chakula na malighafi ambazo zinatumika kuendesha viwanda vyao, kwa mfano, kuzarosha pamba, kahawa (chai) mainchi, katani.

Dini, ili kuwafanya waafrika kuwa na moyo wa kusamehe, na kuwaunda kwa jamii na kuwafanya wawweze kustaarabika, mpango, wamaisha dini ya kikristo (The church missionaries centre)

Ufugaji, ili waweze kupata malighafi za viwandani kwao, mfano, ngozi, pembe, na nyama kwajili ya kitoweo.

Kwahiyo mitaala hiyo iliweza kusaidia sana katika kuleta maendeleo katika jamii mfano kukua kwa mji, masoko, na jumla ya sekta zote za kiuchumi.


Kielelezo Na. 9.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 9.

Kielelezo Na. 9.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kufafanua maudhui yaliyomo katika mtaala wa kufundishia katika shule za wamisionari.

Watahiniwa (11.5%) waliokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu walikuwa na mapungufu mbalimbali katika majibu yao. Mapungufu hayo ni pamoja na kushindwa kutoa maelezo sahihi, kutoa hoja chache na kuchanganya maelezo sahihi na yasiyo sahihi.

Kwa upande mwingine, uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa (80.0%) waliokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu walishindwa

kufafanua maudhui yaliyomo katika mtaala wa kufundishia katika shule za wamisionari kama ilivyooneshwa katika Kielelezo Na. 9.2.


9. i) Utangulizi
ii) Malengo ya mtaala
iii) lugha itakayotumika kufundishia na kujifunzia
iv) Muda wa mafunzo
v) Njia za kufundishia na kujifunzia
vi) Maendeleo ya upimaji

Kielelezo Na. 9.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 9.

Kielelezo Na. 9.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kufafanua maudhui yaliyomo katika mtaala wa kufundishia katika shule za wamisionari. Mtahiniwa aliandika mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa mtaala badala ya kufafanua bayana mambo yaliyopo katika mtaala wa kufundishia katika shule za wamisionari.


### 2.1.10. Swali la 10: Elimu Jumuishi

Swali hili lilipima uelewa wa watahiniwa juu ya faida za kuwepo kwa elimu jumuishi nchini Tanzania. Swali liliuliza:

*Bainisha faida nne za kuwepo kwa Elimu Jumuishi nchini Tanzania.*

Swali hili lilitoka katika mada ya Elimu Jumuishi katika kipengele cha dhana ya elimu jumuishi.

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa watahiniwa 2,738 (81.0%) walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 4. Aidha, watahiniwa 400 (12.0%) walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 2 hadi 2.5; na watahiniwa 223 (6.6%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 1.5. Kwa ujumla kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa wengi (93.4%) walipata alama kuanzia 2 hadi 4. Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 10.




**Chati Na. 10:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 10.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa (81.4%) waliokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu waliweza kubainisha faida nne za kuwepo kwa elimu jumuishi nchini Tanzania. Matokeo ya uchambuzi huu yanadhihirisha kuwa watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu umuhimu wa kuwepo kwa elimu jumuishi nchini Tanzania kama vile : *Kuleta usawa kwa wanafunzi wote, kuondoa unyonge, kuzuia kuzuka kwa matabaka, kutoa fursa kwa wenye mahitaji maalum kupata msaada, kuleta upendo, kujenga ushirikiano* na *kuondoa unyanyapaa*. Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu vizuri swali hili.

10. Faida za Elimu jumuishi Tanzania.
(i) Husaidia kutoa elimu iliyo sawa kwa wanafunzi wote wenye mahitaji maalum na wasio na mahitaji.

(ii) Husaidia kuondoa ubaguzi kati ya wanafunzi wenye mahitaji maalum na wasio na mahitaji.

(iii) Husaidia kujenga ushirikiano na upendo kuanzia shuleni kwa watoto wote ambao wana mahitaji maalum na wasio na mahitaji.


(iv) Huwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalum kupata msaada wa karibu kutoka kwa wanafunzi wenzao wasio na mahitaji maalum.

Kielelezo Na. 10.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 10.

Kielelezo Na. 10 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kubainisha faida za kuwepo kwa elimu jumuishi nchini Tanzania.

Hata hivyo, watahiniwa (12.0%) waliokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu, walitoa hoja pungufu na wengine kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi hivyo kupata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa (6.6%) waliokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu walishindwa kuelewa matakwa ya swali, kwani waliandika hoja pungufu na wengine walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika. Kielelezo Na. 10.2. ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


10. Faida za kuwepo kwa elimu jumuishi nchini tanzania.
1. Husaidia kutatua changamoto za kielimu kwa jamii
ii. Hupelekea kukua kwa stadi mbalimbali za kielimu nchini tanzania.
iii. Husaidia uboreshwaji wa sekta ya elimu katika nchi ya tanzania.
iv. Hupelekea kuongezeka kwa wataalamu wa-elimu nchini Tanzania.

Kielelezo Na. 10.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 10.

Kielelezo Na. 10.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kubainisha faida nne za kuwepo kwa elimu jumuishi nchini Tanzania. Majibu ya mtahiniwa yalikuwa yamelenga uboreshwaji wa jumla wa elimu badala ya faida za uwepo wa elimu jumuishi nchini Tanzania.

## 2.2 SEHEMU B: Saikolojia ya Elimu


Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili ya kujieleza; swali la 11 na swali la 12. Kila swali lilikuwa na alama 15. Watahiniwa walitakiwa kujibu swali 1.

### 2.2.1. Swali la 11: Nadharia za Kujifunza

Swali lilipima uelewa wa watahiniwa juu ya mbinu anazoweza kutumia mwalimu katika kuwamotisha wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Swali liliuliza:

*Chambua mbinu sita anazoweza kutumia mwalimu katika kuwamotisha wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.*
Swali lilitoka katika mada ya Nadharia za Kujifunza katika mada ndogo ya motisha na vichocheo.

Takwimu za uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa zinaonesha kuwa watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa 1,266 sawa na asilimia 75 ya watahiniwa wote. Kati yao, watahiniwa 544 (43.0%) walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 10.5 hadi 14 na watahiniwa 413 (32.6%) walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Aidha, watahiniwa 309 (24.3%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 5.5. Kwa ujumla kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 957 (75.6%) walipata alama kuanzia 6 hadi 15. Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 11.




**Chati Na. 11:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 11.*

Kulingana na matokeo ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa, watahiniwa (43.0%) waliokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu waliweza kuchambua mbinu sita anazoweza kutumia mwalimu katika kuwamotisha wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na uelewa wa kutosha katika mada husika na uelewa mzuri wa matakwa ya swali. Wengi kati yao waliandika utangulizi uliojitosheleza na maelezo sahihi ya

kutetea hoja zao. Kielelezo Na. 11.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu vizuri swali hili.

11 Ufundishaji ni kitendo cha kuwasilisha maarifa, stadi na mielekeo iliyoandaliwa kwa wanafunzi au walengwa, mwalimu anaweza kutumia mbinu mbalimbali katika kuwavutia wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji, zifuatazo ni mbinu hizo:

Motisha chanya, kwa kutumia zawadi kama kuwapigia makofi, vitu halisi, mfano kuwapatia wanafunzi zawadi ya madaftari kwa kufanya vizuri katika kujibu mtihani au maswali.

Kuwashirikisha wanafunzi, kwa kutumia mbinu kama maswali na majibu, majadiliano mwalimu anaweza kuwavutia wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji darasani.

Kutoa mitihani na majaribio ya darasani mara kwa mara, kutoleana na wanafunzi kufanya mitihani na kutambua uwezo wao watapenda sana kujifunza zaidi ili waweze kufaulu au kufanya vizuri katika mitihani yao.

Matumizi ya zana, mwalimu ili aweze kuwavutia wanafunzi katika ufundishaji wake lazima matumizi ya vifaa na zana ambazo zitarahisisha ufundishaji zitumike, Mfano Matumizi ya michoro katika kufundisha mada ya ramani, Matumizi ya vitu halisi kama vijiti, vizibo katika kusoma namba.

Kujenga mahusiano mazuri na wanafunzi; mwalimu kwa kutumia uhusiano huo kuweza kuwasikiliza wanafunzi matatizo yao na kuweza kuyatatua hivyo itasaidia wanafunzi kupenda kujifunza zaidi.

Kutumia mifano mingi wakati wa ufundishaji. Mwalimu kwa kutumia mifano ambayo huweza kupatikana kwa urahisi katika mazingira yanayomzunguka mwanafunzi itasaidia wanafunzi kupenda kujifunza kwa kuvutiwa na ufundishaji wa mwalimu.


Hivyo basi; Mwalimu kwa kutumia mbinu zilizotajwa hapo juu itasaidia wanafunzi kuvutiwa katika mchakato wa ufundishaji kuweza kupata stadi ya kujiamini kwa kushirikishwa, ushirikiano mzuri na wanafunzi wenzake, kuwa na maadili mema katika mchakato wa kujifunza kwa kuweza kutatuliwa matatizo yake na Mwalimu.

Kielelezo Na. 11.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 11.

Kielelezo Na. 11.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kuchambua mbinu mbalimbali anazoweza kutumia mwalimu katika kuwamotisha wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Mtahiniwa aliweza kutoa majibu sahihi hivyo kuwa na ufaulu mzuri katika swali hili.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa (32.6%) waliokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu waliandika utangulizi na hitimisho ambavyo havikujitosheleza. Aidha, walishindwa kuchambua kwa kina mbinu anazoweza kutumia mwalimu katika kuwamotisha wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Kwa upande mwingine, tathmini ya uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa inaonesha kuwa watahiniwa (24.3%) waliokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu walishindwa kuchambua mbinu anazoweza kutumia mwalimu katika kuwamotisha wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Watahiniwa walitoa hoja chache na wengine walichanganya ama kurudia hoja, hivyo kutokukidhi mahitaji ya swali kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 11.2.


11 Mbinu ni njia anazotumia mwalimu katika
mchakato wa kufundishia na kujifunzia. Kuna
aina mbalimbali za mbinu za kujifunzia. kama vile
Kazi mradi, maswali na majibu, Majadiliano katika
vikundi. Zifuatazo ni mbinu anazoweza kutumia
mwalimu katika kuwamotisha wanafunzi katika
mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.
Majadiliano katika vikundi, Mwalimu anaweza
akatumia mbinu ya majadiliano kwa kuwa
majadiliano huamsha ari ya kujifunza kwa
wanafunzi kwani kila mwanafunzi hushiriki
kikamilifu.
Maswali na Majibu, Pia mbinu hii mwalimu
anaweza kutumia katika kuwamotisha
wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na
ujifunzaji kwa kuwa hujenga usikivu pia uamsho
ari ya kujifunza. Pia hii ni miongoni mwa motisha
ambayo mwalimu anaweza kutumia ili kukami
lisha tendo la ufundishaji na ujifunzaji.
Kazi mradi Mwalimu anaweza akatumia

Kielelezo Na. 11.2: Sampuli ya jibu lisilokidhi mahitaji katika swali la 11.

Kielelezo Na. 11.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa ambalo halikukidhi mahitaji ya swali. Swali lilimtaka mtahiniwa kutoa hoja sita lakini mtahiniwa alitoa hoja mbili tu ambazo zinajirudia kwani zipo katika hoja moja ya matumizi ya zana na njia mbalimbali zenye kuamsha ari ya ujifunzaji.


### 2.2.2. Swali la 12: Makuzi na Ukuaji wa Mtoto

Swali hili lilikusudia kupima uwezo wa watahiniwa katika kueleza kasoro sita zinazosababisha mtoto kuwekwa kwenye kundi la kuvia akili. Swali liliuliza:

*Eleza kasoro sita zinazosababisha mtoto kuwekwa kwenye kundi la kuvia akili.*


Swali hili lilitoka kwenye mada ya Makuzi na Ukuaji wa Mtoto katika mada ndogo ya hatua za makuzi ya mtoto.

Takwimu za uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa zinaonesha kuwa watahiniwa 2,090 sawa na asilimia 62.15 ya watahiniwa wote, walifanya swali hili. Kati yao, watahiniwa 1,523 (72.9%) walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 10.5 hadi 14. Aidha, watahiniwa 506 (24.1%) walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10; na watahiniwa 61 (2.9%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 5.5. Kwa ujumla kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa wengi (97.1%) walipata alama kuanzia 6 hadi 15. Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 12.




**Chati Na. 12:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 12.*

Tathmini ya uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa inaonesha kuwa watahiniwa (72.9%) waliokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu waliandika utangulizi unaoendana na swali. Aidha, watahiniwa walieleza kasoro zinazosababisha mtoto kuwekwa kwenye kundi la kuvia akili. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kasoro hizo ambazo ni pamoja na: *utendaji wa akili kuwa chini ya wastani, kupungukiwa stadi za kijamii, kuwa nyuma katika hatua za ukuaji kimwili ikilinganishwa na wenzake, kuwa na uwezo mdogo wa kukumbuka mambo, kuwa mzito katika utendaji* na *kuwa na utukutu wa kutotulia na kuzingatia jambo moja kwa muda mrefu*. Kielelezo Na. 12.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kutoa majibu sahihi katika swali hili.



12. Kuvia akili ni kitendo cha akili ya mtoto kuathiriwa. Kuna sababu mbali mbali zinazoweza kupelekea akili ya mtoto kuvia, sababu hizo ni kama ukosefu wa chakula bora, ajali, maradhi mbali mbali kama polio, kifafa kikuu, nyumbo nya kuzalishia vina weza kuminya ubongo wa mtoto, kukosa hewa ya Oksijeni wakati wa kuzaliwa, msongo wa mawazo. Zifuatazo ni kasoro zitakazo sababisha mtoto kuwekwa kwenye kundi la kuvia akili.

Kuwa na utukutu na kutotulia na kitendo cha aina moja. Watoto wengi waliovia akili huweza kuwa na utukutu na kutofanya kitendo cha aina moja kwa muda mrefu kwa mfano anapokuwa shuleni anaweza kufanya vitendo vingi kwa wakati mmoja mfano kucheza juu ya dawati wakati huohuo kupanda dirishani, wakati huohuo kuchokoza na wenzake.

Kuwa na usikivu mdogo. Mtoto aliyevia akili hukosa usikivu na hawezi kutulizwa au kukatazwa jambo na kuwa na usikivu wa moja kwa moja, lazima aweze kuudhia jinsi ya hali aliyo nayo katwaza.

Kuwa na uzito katika kukumbuka jambo, kukumbuka ni kitendo cha kurudisha au kuleta jambo katika ubongo pindi linapohitajika. Mtoto aliyevia akili hawezi kutiririsha jambo alilojifunza awali katika ubongo wake. na kama

Kielelezo Na. 12.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 12.

Kielelezo Na. 12.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kueleza kwa usahihi kasoro zitakazosababisha mtoto kuwekwa kwenye kundi la kuvia akili. Mtahiniwa ameonesha kuwa na uelewa juu ya mada ya elimu jumuishi hasa katika kipengele cha ulemavu wa akili.

Kwa upande mwingine, watahiniwa (24.2%) waliokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu walishindwa kutetea hoja zao vizuri. Wengine walitoa hoja pungufu ya zile zilizohitajika kwenye swali, kushindwa kuandika utangulizi na hitimisho pamoja na kukosa maarifa juu ya mpango mzuri wa uandishi wa insha.

Aidha, watahiniwa (2.9%) waliokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya kasoro zinazosababisha mtoto kuwekwa kwenye kundi la kuvia akili. Baadhi yao walitoa maelezo yasiyotetea hoja zao, kutoa sababu za kuvia akili badala ya kasoro zinazosababisha mtoto kuwekwa kwenye kundi la kuvia akili. Aidha, wengine walishindwa kutoa utangulizi na hitimisho zuri na hivyo kupata alama hafifu. Kielelezo Na. 12.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuelewa matakwa ya swali katika swali la 12.

12 Makuzi ya mtoto ni suala la kiyamii linalohusu ukuaji na mabadiliko ya mtoto kitabia, kiakiki, kiakili, kihaiba na kimaadili. Kuvia akili ni kitendo cha akili ya mtoto kushindwa kupambanua mambo mbalimbali yanayotokea, ufundishaji na kujifunza kwake. Zifuatazo ni kwiyoro zitakazosababisha mtoto kuwekwa kwenye kundi la kuvia akili:-

Ukosefu wa malezi bora wakati wa ukuaji (malezi duni). Suala la malezi katika ukuaji wa mtoto ni suala nyeti sana linalohusisha malezi ya mtoto kwa kutegemea pande mbili. Malezi yanapokosekana yaani malezi ya baba na mama huleta matokeo hasi katika ukuaji wa akili kwa mtoto na kusababisha kuvia kwa akili.

Ukosefu wa lishe bora kwa mtoto. Kipindi cha ukuaji wa mtoto unaenda sambamba na lishe bora kwa mtoto itakayomwezesha kukua kulingana na mtazamo chanya uliyotegemewa na jamii. Kwa kukosa lishe bora husababisha kushuka kwa uwezo wa akili kuchanganua mambo mbalimbali katika akili.

Matumizi (utumiaji) ya dawa za kulevya. Baadhi ya madawa huweza kusababisha kuharibika au kuvia kwa akili ya mtoto kipindi cha makuzi yake. Mzazi anapotumia dawa za kulevya kama vile bangi, pombe na sigara husababisha kuathirika kwa akili ya mtoto wakati wa makuzi au ukuaji wake. Hivyo kutokana na matumizi ya madawa hayo husababisha akili ya mtoto kuvia.

Magonjwa mbalimbali hatarishi. Pia kuna baadhi ya magonjwa ambayo huweza kusababisha kuvia kwa akili ya mtoto. Magonjwa hayo huathiri mfumo mzima wa ujifunzaji wa akili ya mtoto na huyo kushindwa kupambanua masuala mbalimbali kiakili kwani mfumo mzima wa akili unakuwa umeathiriwa.

Matumizi ya mionzi. Baadhi ya matumizi ya mionzi mbalimbali kama vile X-rays, Ultra sounda na mionzi mingine ni hatari katika ukuaji wa mtoto kwani huenda kuathiri mfumo ya akili.

Mtoto kushindwa kuvumbua dhana ya mambo tofauti katika ujifunzaji (Taahira wa akili). Kasoro hii hupelekea mtoto kuwekwa kwenye kundi la kuvia akili, kwani atakosa uwezo wa kuvumbua silabi, maneno na sentensi kwenye akili yake.

Kwahiyo, kasoro hizi zinazopelekea mtoto kuwekwa kwenye kundi la kuvia akili, huweza kuepukwa kwa kufanya mafunzo, kupata lishe bora kipindi chote cha makuzi, kufanya mazoezi mara kwa mara na kupata malezi bora kutoka kwa wazazi.

Kielelezo Na. 12.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 12.

Kielelezo Na. 12.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza kasoro zitakazosababisha mtoto kuwekwa kwenye kundi la kuvia akili. Jibu la mtahiniwa lilijikita katika kueleza sababu zinazopelekea mtoto kuvia akili badala ya kasoro ambazo zingemtambulisha mtoto aliyevia akili.

## 2.3 SEHEMU C: Mitaala na Ufundishaji

Sehemu C ilikuwa na maswali mawili, swali la 13 na swali la 14. Kila swali lilikuwa na alama 15. Mtahiniwa alitakiwa kujibu swali moja.

### 2.3.1 Swali la 13: Ufundishaji


Swali hili lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu umuhimu wa utoaji wa mazoezi, majaribio na mitihani katika kufanikisha malengo ya kufundisha na kujifunza. Swali liliuliza:

*Kwa kutumia hoja sita, onesha umuhimu wa utoaji wa mazoezi, majaribio na mitihani katika kufanikisha malengo ya kufundisha na kujifunza.*

Swali hili lilitoka kwenye mada ya Upimaji katika Elimu katika mada ndogo ya dhana ya upimaji katika elimu.

Kulingana na takwimu za uchambuzi wa majibu ya watahiniwa, swali hili lilijibiwa na watahiniwa 3,347 sawa na asilimia 99.5 ya watahiniwa wote. Kati yao, watahiniwa 2,231 (69.6%) walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 10.5 hadi 14.5 na watahiniwa 1,008 (30.1%) walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Aidha, watahiniwa 8 (0.2%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 2 hadi 5.5. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa swali hili ndilo lililokuwa

na kiwango kizuri zaidi cha ufaulu katika maswali yote ya insha kwani asilimia 99.7 walipata alama kuanzia 6 hadi 14.5. Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili kimeoneshwa katika Chati Na. 13.




**Chati Na. 13:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 13.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa (69.6%) waliokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 10.5 hadi 14.5 waliweza kuonesha umuhimu wa utoaji wa mazoezi, majaribio na mitihani katika kufanikisha malengo ya kufundisha na kujifunza. Kielelezo Na. 13.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.

13 Kufundisha ni mchakato wa mwalimu kuweza kuandaa maarifa na kuwasilisha kwa mwanafunzi na kujifunza ni kitendo cha kuweza kupokea au kupata maarifa, stadi na mielekeo ambayo huleta badiliko la kudumu; kuna umuhimu wa utoaji wa mazoezi, majaribio na mitihani katika ufundishaji na ujifunzaji. Ufuatao ni umuhimu huo:-

Kutambua kufikiwa au kutofikiwa kwa lengo mahususi; humsaidia mwalimu katika kuweza kumpima mwanafunzi kwa kile alichokusudiwa kukipata kama amepata kwa kulinganisha matokeo ya mazoezi, majaribio na mitihani.

Husaidia wanafunzi kuelewa kiwango chao cha uelewa, kila mwanafunzi atapata alama kutegemeana na uwezo wake wa uelewa na kuweza kufanya jitihada kutokana na alama atakazopata.

Husaidia kutoa motisha kwa wanafunzi; wanafunzi watapenda zaidi kujifunza kwa kupata alama za juu na wale wa alama za chini kuweza kuongeza bidii katika kujifunza hivyo huwavutia wanafunzi kupenda sana kujifunza wanapowekewa alama za majaribio.

Husaidia Mwalimu kutathmini njia na mbinu zake za ufundishaji; kutokana na matokeo yatakayotoka yakiwa mazuri njia zake zitakuwa bora na matokeo yakiwa hafifu itamwezesha katika uboreshaji wa mbinu zake za ufundishaji.

Kutambua matatizo ya wanafunzi na kuweza kuyatatua, mazoezi, majaribio na mitihani huweza kutumiwa na mwalimu katika kutambua matatizo ya wanafunzi na namna ya kuyatatua katika ufundishaji. Mfano mtoto kushindwa kupangilia kazi ya jaribio kwa usahihi na kumuelekeza.

Husaidia kutoa ripoti ya matokeo ya mwanafunzi hii husaidia wazazi kuweza kutambua uwezo wa watoto wao katika ufundishaji na ujifunzaji ambao huweza kuchangia maoni yao kupitia katika matokeo hayo.


Kwa ujumla zana hizo za upimaji ambazo ni mazoezi, majaribio na mitihani katika kufanikisha lengo la ufundishaji ni muhimu sana kwa mwanafunzi, mwalimu, mzazi na jamii kwa kusaidia shule katika kumpandisha mwanafunzi darasa au ngazi; husaidia kulinganisha shule moja na nyingine, lakini mambo ya kuzingatia katika zana hizo mfano ziendane na umri wa walengwa, uelewa, ngazi ya elimu waliyopo ili kufanikisha upimaji huo.

Kielelezo Na. 13.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 13.

Kielelezo Na. 13.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kuonesha umuhimu wa utoaji wa mazoezi, majaribio na mitihani katika kufanikisha malengo ya kufundisha na kujifunza. Mtahiniwa alikuwa na uelewa juu ya mada ya upimaji hasa umuhimu wa utoaji wa mazoezi, majaribio na mitihani katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa (30.1%) waliokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu waliweza kuonesha umuhimu wa utoaji wa mazoezi, majaribio na mitihani katika kufanikisha malengo ya ufundishaji na ujifunzaji. Wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi, kuandika hoja pungufu, na wachache kati yao walishindwa kuelezea vizuri hoja na hivyo kupata alama pungufu.

Aidha, watahiniwa (0.2%) waliokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu walishindwa kutambua matakwa ya swali na wengi wao walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya umuhimu wa utoaji wa mazoezi, majaribio na mitihani katika kufanikisha malengo ya ufundishaji na ujifunzaji. Wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Kielelezo Na. 13.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutoa jibu sahihi katika swali hili.


13 Upimaji ni kitendo cha kuangalia ni kwa kiasi gani mtoto ameelewa kutokana na kile alichofundishwa, umuhimu wa utoaji wa majaribio mitihani.
Humsaidia mwalimu kujua tabia na mwenendo wa mwanafunzi.
Humsaidia mwalimu kupanga matokeo ya wanafunzi.
Husaidia kujua njia na mbinu za kufundishia

Kielelezo Na. 13.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 13.

Kielelezo Na. 13.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuonesha umuhimu wa utoaji wa mazoezi, majaribio na mitihani katika kufanikisha malengo ya kufundishia na kujifunzia. Mtahiniwa alitoa hoja tatu zisizo sahihi kati ya hoja sita alizotakiwa kutoa.


### 2.3.2 Swali la 14: Maendeleo ya Elimu Tanzania

Swali hili lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu malengo ya sera mpya ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014. Swali liliulliza:

*Chambua malengo sita ya sera mpya ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014.*

Swali hili lilitoka katika mada ya Maendeleo ya Elimu Tanzania katika mada ndogo ya historia ya elimu Tanzania.

Watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa 27 sawa na asilimia 0.8 ya watahiniwa wote. Kati yao, watahiniwa 12 (44.4%) walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 10.5 hadi 13 na watahiniwa 12 (44.4%) walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Aidha, watahiniwa 3 (11.1%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 5.5. Kwa ujumla kiwango cha ufaulu wa watahiniwa waliojibu swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa 24 (88.8%) walipata alama kuanzia 6 hadi 15. Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 14.




**Chati Na. 14:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 14.*

Takwimu za uchambuzi wa majibu ya watahiniwa zinaonesha kuwa watahiniwa wengi (99.2%) hawakujibu swali la 14. Hii inaweza kutokana na wanachuo

kutokuwa na utamaduni wa kujisomea makala na machapisho mbalimbali hasa yale yanayotokana na mabadiliko mbalimbali yanayotokea katika sekta ya elimu nchini. Aidha, asilimia ndogo ya watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu.

Watahiniwa (44.4%) waliokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu waliweza kuchambua kwa wastani malengo ya sera mpya ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014. Malengo hayo ni pamoja na: *Kuweka mfumo na miundombinu nyumbulifu yenye kumwezesha mtanzania kujiendeleza kitaaluma, Kutoa elimu na mafunzo yenye viwango na ubora unaotambulika kikanda na kimataifa, Upatikanaji wa fursa mbalimbali za kielimu* pamoja na *Kuongeza rasilimali watu kulingana na vipaumbele vya Taifa.* Malengo mengine ni*: Usimamizi na uendeshaji madhubuti wa elimu ikiwa ni pamoja na usimamizi wa utekelezaji wa mitaala, Kujenga mifumo endelevu ya ugharimiaji wa elimu na mafunzo nchini ikiwemo utoaji wa elimu ya msingi bure* na *Kujenga mfumo imara wa elimu unaozingatia masuala mtambuka.* Baadhi yao walishindwa kutoa maelezo ya kina kutetea hoja zao. Pia utangulizi pamoja na hitimisho havikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na hoja husika. Aidha, hoja walizotoa zilikuwa zinajirudia. Kielelezo Na. 14.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetoa hoja zenye mwelekeo wa matakwa ya swali.

14. Sera ya elimu ni muongozo katika utoaji wa elimu katika nchi. Kila nchi ina sera ya elimu ili kuboresha elimu kwa wananchi ili kupunguza umbali wa kutu- wasijue kusoma na kuandika na kupunguza ujinga na umaskini kwa wananchi. Yafuatayo ni malengo ya sera ya elimu ya mwaka 2014.

Kuinua ubora wa elimu. Katika sera ya mwaka 2014 malengo yake makuu ni kuinua elimu. Tanzania, kuongeza ubora na kuboresha baadhi ya mahitaji ya elimu ili wananchi wapate elimu iliyo bora.

Kutoa fursa za elimu kwa usawa, katika kipindi cha nyuma baadhi ya kupata uhuru baadhi ya jamii zilikuwa hazipati elimu hivyo katika sera ya mwaka 2014 imetaka kila mwananchi awe na fursa sawa katika kupata elimu.

Kuinua ubora wa mitaala ya shule ili kufikia mahitaji ya sera ya taifa ya elimu, katika kipindi hichi cha sera ya 2014 imetaka kuboresha mitaala na kuondoa mapungufu yote yaliyopo ili kutoa elimu kwa ufanisi na inayoendana sera ya taifa na mahitaji ya jamii.

Kuendeleza matumizi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza katika ufundishaji au utoaji wa mafunzo katika sera hii imetaka kuwe na matumizi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza katika ngazi zote za elimu ili kukuza lugha ya Kiswahili.

Kuinua na kuboresha upimaji na tathmini katika ngazi zote za elimu, sera hii ina lengo la kuboresha ili kutatua kujua maendeleo ya wanafunzi.

Kutoa elimu ya msingi kwa wote kikamilifu; Miongoni mwa malengo mengine ya sera ya mwaka 2014 ni kusisitiza kuhusu utoaji wa elimu ya msingi kwa wote ili kuinua ujuzi na maarifa na kukuza fikra kwa wananchi ili kuleta maendeleo katika jamii.

Hitimisho, malengo ya sera hii ni kuongeza ubora wa elimu katika nchi ili kuongeza maendeleo yenye hadhi na tija katika jamii.

Kielelezo Na. 14.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 14.

Kielelezo Na. 14.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyekuwa na uelewa kuhusu sera ya elimu ya mwaka 2014. Aidha, mtahiniwa alichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na pia kutoa hoja zenye kujirudia hivyo kushindwa kupata alama zote katika swali hili. Mtahiniwa alionesha kuwa na uelewa juu ya Sera ya Elimu ya Mwaka 2014. Hata hivyo, hoja ya mtahiniwa kuwa lengo mojawapo la sera ya elimu ni *kuendeleza matumizi ya lugha ya kiswahili na kiingereza*, haikuwa sahihi.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa (44.4%) waliokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu waliweza kutoa hoja chache zilizokuwa sahihi. Aidha, utangulizi na hitimisho havikuendana na matakwa ya swali.

Kwa upande mwingine, watahiniwa (11.1%) waliokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu walishindwa kuelewa matakwa ya swali na wengi wao walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya Sera ya Elimu ya Mwaka 2014. Kielelezo Na. 14.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutoa jibu sahihi katika swali hili.

14 Elimu ni jumla ya mambo yote yanayotamalimia na mila na desturi za jamii ambayo mtu huweza kupata kwa kufundishwa, kujifunza mwenyewe na kwa njia nyingineyo. Yafuatayo ni malengo ya sera mpya ya Elimu na mafunzo ya mwaka 2014.

Husaidia kukuza vipaji mbalimbali, hii ni kwa sababu watu wengi huwa na vipaji ambavyo hivivi haviji endelea hivyo elimu inavyotolewa humsaidia kukuza kipaji chake.

Husaidia kudumisha utamaduni wa nchi na imani, elimu inapotolewa kwa watu humsaidia kudumisha imani na utamaduni wao kwa kufuata utaratibu uliopo katika mazingira yao.

Husaidia wananchi kuendana na wakati, elimu inapotolewa huwasaidia wananchi waendane na wakati uliopo mfano teknolojia inayotumika katika kipindi kwa wagonjwa hospitalini.

Husaidia kuwafanya watu wajitambue na kujiamini, elimu ambayo hupewa watu huweza kuwafanya wajitambue na kujiamini kutokana na kazi wanazofanya mfano mjasiliamali. wa uzalishaji wa mboga na matunda

Husaidia kufanya watanzania wajitegemea, elimu inawezesha kufanya watanzania wajitegemea kutokana na kazi mbalimbali za uzalishaji ambazo hufanya kwa ajili ya maendeleo yao.

Husaidia kuongeza ajira, elimu inayotolewa huwezesha kuongeza ajira mbalimbali kwa watu mfano walimu, ambao huwa inafuata miiko ya kazi.

Kwa ujumla elimu na mafunzo ya mwaka 2014 inakumbana na changamoto za ukosefu wa vifaa na wataalamu wa kutoa mafunzo na elimu hiyo.

Kielelezo Na. 14.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 14.

Kielelezo Na. 14.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuchambua malengo ya sera ya Sera ya Elimu ya Mwaka 2014. Mtahiniwa alionekana kuwa na uelewa hafifu juu ya sera hii na pia uwasilishaji wa hoja zake haukuwa mzuri kwani malengo hayawezi kuwasilishwa kwa kuanza na neno "husaidia". Uwasilishaji huu unaonesha kuwa mtahiniwa alielewa kuwa swali lilimtaka kutoa umuhimu wa Sera ya Elimu badala ya malengo ya sera husika.

## 2.4 SEHEMU D: Utafiti wa Kielimu, Upimaji na Tathmini

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili, swali la 15 na swali la 16. Kila swali lilikuwa na alama kumi na tano ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu swali moja.


### 2.4.1 Swali 1a 15: Upimaji katika Elimu

Swali hili lilipima uwezo wa watahiniwa kueleza faida tatu na hasara tatu za maswali ya kuchagua jibu sahihi. Swali liliuliza:

*Maswali ya kuchagua jibu sahihi yana faida na hasara kwa mwalimu na mwanafunzi. Eleza kwa kina hoja hii kwa kuzingatia faida tatu na hasara tatu za maswali ya kuchagua jibu sahihi.*

Swali hili lilitoka kwenye mada ya Upimaji katika Elimu katika kipengele cha utungaji wa majaribio na mitihani.

Takwimu za uchambuzi zinaonesha kuwa watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa 2,987 sawa na asilimia 88.8 ya watahiniwa wote. Kati yao, watahiniwa 1,608 (53.8%) walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa 1,021 (34.2%) walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 10.5 hadi 15; na watahiniwa 358 (12.0%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 5.5. Kwa ujumla kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa wengi (88.0%) walipata alama kuanzia 6 hadi 15 kama inavyoonekana katika Chati Na. 15.




**Chati Na. 15:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 15.*

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa (34.2%) waliokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu waliweza kueleza faida na hasara ya maswali ya kuchagua jibu sahihi. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na waliweza kutambua matakwa ya swali. Kielelezo Na. 15.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu vizuri swali la 15.

15 Maswali ya kuchagua jibu sahihi, ni
maswali ambayo yanamtaka mwanafunzi -
achague jibu moja sahihi katika vichacha
wizi ya majibu, maswali haya huwa na faida
zake na hasara zake katika mchakato mzim
a wa kujifunza na ufundishaji, kwa kuanza
na faida za maswali ya kuchagua jibu sahih
i ni hizi zifuatazo :
Husaidia kupima eneo kubwa la -
maudhui, kutokana na mwalimu anatunga -
maswali kwa kutumia mada mbalimbali -
hivyo eneo kubwa la maudhui hutumimika
tofauti na maswali ya insha ambayo yana
pima eneo dogo la maudhui.
Pia ~~hukuza uwezo wa kukum~~
~~buka~~, ~~uwezo wa kukumbu~~
Pia ni rahisi kusahihisha kwa
mwalimu, maswali haya yana urahisi mkubwa
sana katika kusahihisha ukilinganisha -
na maswali ya insha, hivyo mwalimu huwa
hatumii muda mwingi kusahihisha kutokan
ana majibu anakuwa ameshaandaa taya
ri na huwa ni herufi tu moja hivyo ana
tumia muda mchache sana katika kusahi
hisha.
Pia Maswali haya huokoa muda
, muda unaotumika ni mchache sana katika
usahihishaji na utungaji pia na hata -
kwa mwanafunzi katika kujibu kwasa
babu huwa haandiki bali anachagua tu jib
u moja ambalo ni sahihi, pia maswali ha-
ya pamoja na kuwa na faida lakini pia
yana hasara zake na hasara hizo ni hizi

Ni rahisi kufanya udanganyifu kutokana na kuchagua jibu sahihi mwanafunzi huweza kufanya udanganyifu kwa kuigizia majibu kwa mwanafunzi mwenzake na mwalimu asiweze kutambua kama jibu alioandika ameigilizia.

Ni rahisi kubuni jibu, pia mfongoni mwa kasoro za maswali haya huweza kusababisha mwanafunzi asifikirie zaidi kuandika jibu sahihi na akabuni tu jibu hivyo kutamfanya mwanafunzi ashindwe kushughulisha zaidi akili yake katika kukumbuka.

Pia hayakuzi stadi ya kuandika hiyo ni mfongoni mwa kasoro ya maswali haya hayakuzi stadi ya kuandika ukilinganisha na maswali ya insha, hivyo humfanya mwanafunzi ashindwe kupangila vizuri mtiririko wa mawazo kutoka na kuchagua tu herufi moja ya jibu sahihi.

Hivyo hizo ndizo faida za maswali haya ya kuchagua jibu sahihi pamoja na kuwa ni mazuri Mwalimu hatumii muda mwingi hivyo huweza kusababisha kufanya mambo yake mengine kama kupata muda mwingi wa kuandaa masahihisho na kuandaa somo jengine, lakini pia humduma za mwanafunzi na hufanya muda mwengine kushindwa kujua uwezo wa mwanafunzi kutokana na wanafunzi wengine huwa hawana uaminifu katika kujibu mtihani.

Kielelezo Na.15.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 15.

Kielelezo Na. 15.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeeleza faida na hasara za maswali ya kuchagua jibu sahihi. Hata hivyo hoja ya kuwa utungaji wa *maswali haya hutumia muda mchache* haikuwa sahihi kwani maswali haya hutumia muda mrefu katika kutunga hasa katika kuandaa vichachawizi vyenye sifa.

Watahiniwa (53.8%) waliokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu walitoa hoja pungufu pamoja na ufafanuzi usiokuwa wa kina. Pia baadhi yao walishindwa kutoa utangulizi mzuri na hitimisho zuri na hivyo kupata alama za wastani. Wengine walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa (12.0%) waliokuwa na ufaulu hafifu walishindwa kukidhi matakwa ya swali na wengine walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika. Baadhi yao walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na wengine kushindwa kuelewa matakwa ya swali. Kielelezo Na. 15.2 kinaonesha mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa ufasaha.

15 Maswali ya ~~maji~~ Kuchagua majibu Sahihi,
Ni maswali yanayo mpima mwanafunzi uwezo wa-
Kukumbuka mambo kwa haraka pia husaidia wakati
ka kuwafanya wanafunzi wawoze kuwa na akili
ya kufikiria mambo kwa upana zaidi zifuatazo
zo ni ni faida na hasara kwa mwalimu na-
mwanafunzi za maswali ya majibu ya kuchagua.
Humsaidia mwalimu na mwanafunzi kuwa na
Kumbukumbu juu ya mambo fulani, Maswali ya ma
jibu kuchagua majibu sahihi ni maswali yanayo uoza
Kumfanya mwalimu na mwanafunzi kuwa na uwezo mk
bwa wa kufikiri mambo na kuyapambanua kiundani
zaidi.
Humsaidia mwanafunzi kuweza kujibu masw
ali mengine, hii ni kutokana na kumpa mwanga ju
ya maswali yasiyo kua na majibu ya kuchagua na
Kumfanya mwanafunzi awoze kukumbuka mambo kw
a haraka.
Humsaidia mwaumu kujua aina gani ai to
ya maswali ni bora zaidi ya kutoa katika-
mazoezi, majaribio na mitihani, hii ni kutokana na
kuwajua wanafunzi wake juu ya maswali wanayo
weza kuyafanya kwa ufasaha zaidi na namna
gani atuweza kuwashauri juu ya uchaguzi bora w
a maswali.

Zifuatazo ni hasara za maswali ya kuchagua
jibu lisilo sahihi,
Humfanya mwanapunzi kushindwa kujibu m
aswali atakayo ulizwa papo kwa hapo (ana kwa ana),
hii ni kutokana na wanafunzi kukariri na kushi
ndwa kutafakari mambo kwa haraka
Humsaidia mwalimu kujua kama ameele
weka katika somo, kila mwalimu hufundisha kw
a lengo la kutoa maarifa kwa wanafunzi wako ili
wawoze kuyatumia maarifa hayo katika kufanikish
a utatuzi wa changamoto wanazo kumbwa nazo-
hivyo basi mwalimu atuweza kujua kwa kama wana
funzi wake wamemuelewa kwa kutoa majaribio, mazoezi
na mitihani.
Humsaidia mwalimu na mwanafunzi kutunza
Kumbukumbu, juu ya mambo fulani, Mwalimu ana
weza kutunza kumbukumbu za ufaulu wa wanafun
zi katika mitihani, majaribio na mazoezi anayo- wupa
tia wakati mwanafunzi huweza kujitunzia kumbu
Kumbu juu ya mambo aliyo jitunza ~~na~~ au kutund
rshwa na mwalimu na kupelekea ~~mwalimu~~ mwanafunzi kufa
nya vyema pale anapo kutana na jaribio, m
tihani au zoezi la aina yoyote.

Kielelezo Na. 15.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 15.

Kielelezo Na. 15.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza faida na hasara za maswali ya kuchagua jibu sahihi. Mtahiniwa alichanganya hoja zake kwa kuandika faida upande wa hasara. Hata hivyo, hoja hizo hazikuwa sahihi.


### 2.4.2 Swali la 16: Upimaji katika Elimu

Swali hili lilipima uwezo wa watahiniwa katika kueleza mambo ya kuzingatia wakati wa kumpima mwanafunzi kupitia shughuli za kiutendaji. Swali liliuliza:

*Eleza mambo sita ya kuzingatia wakati wa kumpima mwanafunzi kupitia shughuli za kiutendaji.*

Swali lilitoka kwenye mada ya Upimaji katika Elimu katika mada ndogo ya dhana ya upimaji katika elimu.

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa 369 sawa na asilimia 11.0 ya watahiniwa wote. Kati yao, watahiniwa 144 (38.9%) walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10 na watahiniwa 138 (37.5%) walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Aidha, watahiniwa 87 (23.6%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 5.5. Kwa ujumla, kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa wengi (76.4%) walipata alama kuanzia 6 hadi 15 kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 16.




**Chati Na. 16:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 16.*


Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa (37.2%) waliokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu waliweza kueleza mambo ya kuzingatia wakati wa kumpima mwanafunzi kupitia shughuli za kiutendaji. Aidha, watahiniwa hawa waliweza kuonesha uelewa kuhusiana na upimaji wa wanafunzi hasa upimaji kwa vitendo kwa kutoa majibu yanayoendana na mwongozo wa usahihishaji kwa kiwango kikubwa. Majibu sahihi ya swali hili yalikuwa: *Kuona kama mwanafunzi amesoma maelezo kabla ya kutenda, kuona kama anatumia vifaa na zana kwa uangalifu, kuonana kama amepata matokeo ya kuridhisha, kuona kama amerudisha vifaa sehemu husika, kuona kama anajitegemea au anategemea wengine katika kukamilisha kazi yake* na *kuona kama ana ujasiri wa kufanya kile anachopaswa kufanya*. Kielelezo Na. 16.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.

16. Shughuli za kiutendaji, hizi ni shughuli mbalimbali ambazo zinajumuisha kufanya matendo mbalimbali mfano majaribio, uchunguzi Ufinyanzi. Kumpima mwanafunzi katika shughuli za kiutendaji tunaangalia uwezo wa mwanafunzi katika kutenda mambo mbalimbali kwa kutumia vifaa mbalimbali. Yafuatayo ni mambo ya kuzingatia wakati wa kumpima mwanafunzi kupitia shughuli za utendaji :- Yafuatayo ni mambo ya kuzingatia wakati wa kumpima mwanafunzi kupitia shughuli za kiutendaji :-

Uwezo wake kutumia vifaa/zana kwa Usahihi, katika kumpima mwanafunzi katika shughuli za kiutendaji tunaangalia uwezo wa mwanafunzi katika kutumia zana je anaitumia zana ipasavyo? Mwanafunzi anaeitumia zana ipasavyo tunasema ana uwezo wa kiutendaji. mfano uwezo wa kutumia darubini kufanya uchunguzi wa kiayoasi

Pia tunazingatia uwezo wake kutumia zana/vifaa kwa uangalifu, tunapompima mwanafunzi katika shughuli za kiutendaji tunaangalia umakini wake katika kutumia, mfano Asidi na majaribio mengine yanahitaji umakini wa hali ya juu ili kuepuka ajali na kupata matokeo sahihi.

Vilevile kuzingatia uwezo wa kupata matokeo/majibu sahihi, katika kupima shughuli za kiutendaji kwa mwanafunzi tunaangalia je amepata matokeo sahihi? Kwasababu lengo la kutumia vifaa kupata




matokeo sahihi. Mfano ikiwa Asidi + Base
Unapata chumvi na maji, basi tunategemea
katika majaribio mwanafunzi apate matokeo
ya chumvi na maji.
Si hivyo tu kuzingatia kama anarudisha
vifaa mahali pake baada ya kuvitumia, katika
Swala nzima la kumpima mwanafunzi kiutendaji
baada yakufanya majaribio tunapima uwezo
wa kurudisha vifaa mahali pake kwasababu
husaidia kuepusha ajari kutokana nakuwa
na mpangilio mbaya wa vifaa hivyo.
Pia kuzingatia kama anajitegemea au
anategemea wengine katika kupata matokeo,
katika kumpima mwanafunzi katika shughuli
za kiutendaji tunaangalia kama anapata
matokeo pekeake au anategemea wengine
hii inasaidia kuwabaini wanafunzi waliweza
kumudu stadi za Utendaji yaani ambao
hawategemei mtu mwingine kupata matokeo.
Vilevile kuzingatia uwezo wa mwanafunzi
kuviweka vifaa katika hali ya usafi baada ya
kuvitumia, mfano katika majaribio ya kisayansi
tunatarajia kuona baada ya majaribio vifaa vinasafishwa
Pia kuzingatia uwezo wa kusoma maelekezo
kabla ya kutenda, hapa tunapima umakini
wa mwanafunzi katika kufanya vitendo.
mfano majaribio ya kisayansi yanatakiwa kufanywa
kwa umakini kwa kufuata maelekezo.
Kiujumla, Mwalimu ~~hed~~ hana budi
kuwa makini anapompima mwanafunzi kiutendaji
kwasababu husaidia kuepusha ajali zisizo za
lazima wakati wa mihakato wa kujifunza.

Kielelezo Na. 16.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 16.

Kielelezo Na. 16.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kueleza mambo ya kuzingatia wakati wa kumpima mwanafunzi kupitia shughuli za kiutendaji. Mtahiniwa alikuwa na uelewa mzuri kuhusu upimaji wa wanafunzi hasa kupitia shughuli za kiutendaji.

Aidha, watahiniwa (38.9%) waliokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu, walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Wengine walishindwa kuelezea vizuri hoja zao.

Kwa upande mwingine, watahiniwa (23.6%) waliokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu, hawakuelewa matakwa ya swali na hivyo kupata alama hafifu kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 16.2.


16 Upimaji: Ni mchakato wa kukusanya, kuunganisha na kutafsiri taarifa mbalimbali kwa ajili ya kutoa maamuzi sahihi.
Yafuatayo ni mambo ya kuzingatia wakati wa kumpima mwanafunzi kupitia shughuli za kiutendaji.
Mazoezi; Ni miongoni mwa mambo ambayo hupelekea kumpima mwanafunzi kupitia shughuli za kiutendaji
Mitihani. Ni miongoni mwa mambo ambayo hupelekea kumpima mwanafunzi kupitia shughuli za kiutendaji ambapo humfanya mwanafunzi kuwa na maendeleo mazuri kitaaluma.
Majaribio. Ni miongoni mwa mambo ambayo hupelekea kumpima mwanafunzi katika shughuli za kiutendaji ambapo humfanya mwanafunzi kuwa na maendeleo mazuri kitaaluma.
Maswali dodoso. Ni miongoni mwa mambo ambayo hupelekea kumpima mwanafunzi katika shughuli za kiutendaji ambapo hupelekea mwanafunzi kuwa na maendeleo mazuri kitaaluma.
Kazi mradi. Ni miongoni mwa mambo ambayo hupelekea kumpima mwanafunzi katika shughuli za kiutendaji kwani humfanya mwanafunzi kuwa na maendeleo mazuri kitaaluma.
Hivyo basi hayo ni miongoni mwa mambo ya kuzingatia wakati wa kumpima mwanafunzi kupitia shughuli za kiutendaji kwani hupelekea matokeo mazuri kwa mwanafunzi katika taaluma yake.

Kielelezo Na. 16.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 16.

Kielelezo Na. 16.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza mambo ya kuzingatia wakati wa kumpima mwanafunzi kupitia shughuli za kiutendaji. Mtahiniwa hakuwa na uelewa wa matakwa ya swali hivyo kuelezea njia za upimaji badala ya mambo ya kuzingatia wakati wa kumpima mwanafunzi kupitia shughuli za kiutendaji.

## 2.5 SEHEMU E: Misingi ya Elimu

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili, swali la 17 na swali la 18. Kila swali lilikuwa na alama 15 ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu swali 1.


### 2.5.1 Swali 1a 17: Uongozi wa Elimu

Swali hili lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu faida za uongozi wa kidikteta. Swali liliuliza:

*Kila aina ya uongozi ina faida na hasara zake. Jenga hoja juu ya kauli hii kwa kutoa faida sita za uongozi wa kidikteta.*

Swali hili lilitoka katika mada ya Uongozi wa Elimu Tanzania katika kipengele cha dhana ya uongozi wa elimu.

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa 1,145 sawa na asilimia 34.0 ya watahiniwa wote. Kati yao, watahiniwa 662 (57.8%) walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu wa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Aidha, watahiniwa 437 (38.2%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu wa kupata alama kati ya 0 na 5.5; na watahiniwa 46 (4.0%) walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu wa kupata alama kuanzia 10.5 hadi 14. Kwa ujumla, kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa wengi (61.8%) walipata alama kuanzia 6 hadi 14. Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 17.




**Chati Na. 17:** *Ufaulu wa watahiniwa katika Swali la 17.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa (4.0%) waliokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu waliweza kueleza faida za uongozi wa kidikteta. Kielelezo 17.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.

17. Uongozi ni mamlaka anayopewa mtu kusimamia jambo fulani. Au ni kitendo cha kueleke za au kuwa juu ya mamlaka. Mtu anayepewa madaraka ya kusimamia jambo anaitwa - kiongozi. Kuna aina nne za uongozi nazo - ni uongozi wa kidikteta, uongozi wa kidemokrasia, uongozi wa Mahusiano mema na uongozi ~~wa~~ uliobweteka.

Uongozi wa kidikteta ni aina ya uongozi ambao kiongozi anakuwa na mamlaka yote na walio chini yake ~~na~~ wanatakiwa kufuata - bila kuhoji wala kupinga. Hii ina maana - kwamba kiongozi ndo anakuwa na madaraka yote pasipo kumshirikisha aliye chini - yake. Uongozi huu wa kidikteta una faida zifuatazo:-

^Husaidia^ Watu kufuata sheria; katika uongozi - huu watu hawana budi kufuata sheria kwa - sababu bila kufuata sheria inapelekea kuadhibiwa kwa kuwa huu ni uongozi wa kimabavu. Kwahiyo watu wote wanatakiwa kufuata - sheria zilizowekwa.

^Hupelekea^ Ufanisi wa kazi; Watu hufanya - kazi kwa bidii katika uongozi huu. Kazi zinafanyika kwa ubora zaidi katika uongozi wa kidikteta hii ni kutokana na kiongozi - kuwa mkali au kuongoza kwa mabavu.

^Husaidia^ Kazi nyingi hufanyika kwa wakati; Wananchi wanafanya kazi zilizopangwa kwa - muda uliopangwa bila kuvuruga ratiba zingine. Hii ni kutokana na kiongozi kuwa - mkali. Watu hufanya kazi kwa wakati kwa

kuogopa adhabu au kwa kumhofia kiongozi. -
kwahiyo kutokana na ukali wa kiongozi
itampelekea afanye kazi kwa wakati.
Huleta maendeleo ya haraka katika jamii; Mae
ndeleo ya haraka yatakuja endapo watu watafa
nya kazi kwa ufanisi na kwa wakati. katika
uongozi huu wa kidikteta watu wanakuwa
na uoga na hofu, hii itapelekea wafanye kazi
kwa bidii, kwa kufanya hivyo itapelekea
maendeleo katika jamii.
Husaidia katika kupunguza uzembe kazini;
Aina hii ya uongozi uzembe kazini hupu
ngua. Hii ni kutokana na wafanyakazi -
kuhofia au kwa kumhofia kiongozi wao.
kiongozi anapokuwa mkali, watu hupunguza
uzembe.
Husaidia kupunguza hasara mbalimbali;
kuna hasara mbalimbali zinazotokea katika
jamii kama vile vifo, kutokana na uongozi -
huu hupunguza hasara hiyo kwa mfano katika
hospitali madaktari watafanya kazi kwa -
bidii ya kuwahudumia wagonjwa hii itasaidia
kupunguza vifo.
Hivyobasi; uongozi wa kidikteta unafa
a sana katika jamii kutokana na faida -
zilizoelezwa hapo juu. pia uongozi huu -
wa kidikteta una hasara katika jamii -
kama vile hujenga chuki, uhasama, matabaka
na kadhalika. Aina hii ya uongozi ni -
nzuri kwa kiasi chake na ni mbaya kwa -
kiasi chake.

Kielelezo Na. 17.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 17.

Kielelezo Na. 17.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyekidhi matakwa ya swali kwa kutoa faida za uongozi wa kidikteta kwa usahihi.

Watahiniwa (57.8%) waliokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu walitoa maelezo ambayo hayakujitosheleza katika kutetea hoja zao. Aidha, wapo walioshindwa kutoa maelezo sahihi katika sehemu ya utangulizi na hitimisho.
Kwa upande mwingine, watahiniwa (38.2%) waliokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu walishindwa kukidhi matakwa ya swali, kushindwa kuandika vizuri

maneno na wengine walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika. Kielelezo Na. 17.2. ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa ufasaha.

17. Uongozi wa kidikteta ni uongozi ambao haufuati mfumo wa kidemokrasia katika utendaji wake wa kazi. Zifuatazo ni hasara za kuwa na mfumo huu wa uongozi wa kidikteta:-

Hauna ushirikishwaji kiutendaji, maamuzi yanakuwa kwa kiongozi akitoa tamko hata lisilofaa linafuatwa bila kupinga kwani kiongozi ndie msemaji wa mambo yote bila kuingiliwa na mwingine.

Unafuata mfumo wa chama kimoja, chama kinakuwa mikononi mwa kiongozi huyo kila jambo wananchi wanatakiwa kufuata utaratibu uliowekwa na chama husika bila kupingwa na chama chochote.

Hakuna uhuru na haki kidemokrasia, hapa uchaguzi wake unakuwa haufuati demokrasia bali unakuwa unatazama zaidi sera ya chama chake huyo hutumia mabavu kuwepo madarakani bila kujali sera ya nchi nzima.

Uongozi hufuata maslahi yake nasio ya nchi nzima, hapa kiongozi wa kidikteta anakuwa zaidi kujitunia yeye kuliko kuisaidia nchi kukuza uchumi na maendeleo mengine mfano Idd amin na benedicto mussolin katika Afrika pia mugabe.

Dola inakuwa chini ya kiongozi husika, wakati dola inatakiwa iwe ya kila mtu lakini kwenye uongozi huu dola huwa chini yake maamuzi yote hutoa hukumu yeye. huyo kero za wana nchi zinaweza zisisikilizwe kabisa.

Shughuli za kimaendeleo zinafanywa kwa amri na kutofuata haki za binadamu, hapa haijalishi mwesana au mlemavu mradi wa utendaji utafikie lazima kila mtu awajibike kisawa sawa. jambo ambalo kulingana na haki za binadamu linakuwa limevuka mipaka.

Hata hivyo uongozi wa kidikteta una faida pia kama vile, kupanga kazi kwa bidii bila ufegevu, kuwa na maamuzi sahihi bila upendeleo, kuendesha dola katika mwongozo binafsi, kutochelewesha suala la kupiga kampeni za kura na kupanga uchaguzi kwa uharaka zaidi.

Kielelezo Na. 17.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 17.

Kielelezo Na. 17.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuelewa matakwa ya swali. Mtahiniwa alitoa hasara za uongozi wa kidikteta badala ya faida za uongozi husika kwa mujibu wa matakwa ya swali.


### 2.5.2 Swali 1a 18: Elimu ya Watu Wazima

Swali lilipima uelewa wa watahiniwa katika kueleza kwa ufasaha mambo yanayoweza kufanya mwanafunzi mtu mzima asiwe na motisha ya kujifunza. Swali liliuliza:

*Kwa kutumia mifano, eleza kwa ufasaha mambo sita yanayoweza kufanya mwanafunzi mtu mzima asiwe na motisha ya kujifunza.*

Swali hili lilitoka katika mada ya Elimu ya Watu Wazima katika kipengele cha dhana ya elimu ya watu wazima.

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa 2,210 sawa na asilimia 65.7 ya watahiniwa wote. Kati yao watahiniwa 1,636 (74.0%) walikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10 na watahiniwa 450 (20.4%) walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 10.5 hadi 14.5. Aidha, watahiniwa 124 (5.6%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 5.5. Kwa ujumla, kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwani watahiniwa wengi (94.4%) walipata alama kuanzia 6 hadi 14.5. Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 18.




**Chati Na. 18:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 18.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa (20.4%) waliokuwa na kiwango kizuri cha ufaulu waliweza kueleza kwa ufasaha mambo yanayoweza kufanya mwanafunzi mtu mzima asiwe na motisha ya kujifunza. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na waliweza kutambua matakwa ya swali. Kielelezo Na. 18.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

18. Kwa kutumia mifano, kueleza kwa ufasaha mambo sita yanayoweza kufanya mwanafunzi mtu mzima asiwe na motisha wa kujifunza.


Mwanafunzi mtu mzima ni mtu alie na umri kuanzia miaka 18 na kuendelea ambaye anajifunza mambo mbalimbali ili yaweze kumsaidia katika maisha yake. Yafuatayo ni mambo sita yanayoweza kufanya mwanafunzi mtu mzima asiwe na motisha ya kujifunza.

Kutothaminiwa. Mwanafunzi mtu mzima anaposhindwa kutathiminiwa na mwalimu wake hukosa motisha ya kujifunza hivyo humuondolea usikivu katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji.

Kutoheshimu mawazo yake. Siku zote mwanafunzi mtu mzima hupenda kuheshimiwa mawazo yake aliyoyatoa hata kama atakua ameenda tofauti. Kwahiyo mwalimu anaposhindwa kuheshimu mawazo ya mwanafunzi mtu mzima hukosa motisha ya kujifunza.

Kufundishwa kwa nadharia bila vitendo. Mwanafunzi mtu mzima hupenda kujifunza kwa vitendo kuliko nadharia hivyo mwalimu anaposhindwa kuwafundisha kwa vitendo hawatokua na motisha katika kujifunza.

Kujifunza vitu ambavyo havimpi manufaa. Mwanafunzi mtu mzima huweza kua na motisha ya kujifunza jambo ambalo anaona lina umuhimu katika maisha



yake hivyo mwanafunzi mtu mzima anapojifunza mambo ambayo hayaleti faida kwake hukosa motisha katika kujifunza.

Kujifunza vitu vigumu. Mwanafunzi mtu mzima hupenda kujifunza vitu virahisi, wanapojifunza vitu virahisi hufurahi sana. Hivyo mwalimu anapofundisha vitu vigumu huondoa motisha ya kujifunza

Mwalimu kutotambua ujuzi alionao. Mwanafunzi mtu mzima hawezi kua na motisha ya kujifunza endapo mwalimu hatotambua kua jambo analofundisha hata yeye analifahamu.

Hivyo ili kuweza kumfanya mwanafunzi mtu mzima aweze kuwa na motisha katika kujifunza lazima mwalimu aheshimu mawazo yao, awathamini, aelewe kua wanapenda kujifunza vitu virahisi pia aweze kuelewa ujuzi walionao katika mambo anayowafundisha.


Kielelezo Na. 18.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 18.

Kielelezo Na. 18.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kueleza kwa ufasaha mambo yanayoweza kufanya mwanafunzi mtu mzima asiwe na motisha wa kujifunza. Mtahiniwa alikuwa na uelewa juu ya mada ya elimu ya watu wazima hivyo kuelewa matakwa ya swali.

Aidha, watahiniwa (74.0%) waliokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu, baadhi yao walitoa maelezo ambayo hayakujitosheleza katika kutetea hoja zao au kutoa baadhi ya hoja zisizo sahihi. Hata hivyo, wapo walioshindwa kutoa maelezo sahihi katika sehemu ya utangulizi na hitimisho.

Kwa upande mwingine watahiniwa (5.6%) waliokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu walishindwa kukidhi matakwa ya swali. Baadhi yao walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika kutumia mifano kueleza kwa ufasaha

mambo yanayoweza kufanya mwanafunzi mtu mzima asiwe na motisha ya kujifunza, kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 18.2.



18. Mwanafunzi mtu mzima ni mwanafunzi ambaye hujifunza mwenyewe bila uhitaji wa kuelekezwa na mtu yeyote kile anachopaswa kujifunza.

Yafuatayo ni mambo yanayo mfanya mwanafunzi mtu mzima asiwe na motisha

Huwa na malengo ya baadae, Mwanafunzi mtu mzima hahitaji kuwa na motisha wakati anapokuwa akijifunza kwani hufanya kitu kwa malengo yake ya baadae.

Hufanya mambo yake mwenyewe bila ya kuamuriwa na mtu yeyote, Mwanafunzi mtu mzima anapokuwa katika kujifunza hahitaji motisha yoyote kwani hufanya mambo yake mwenyewe bila amri yoyote na kwa wakati wake mwenyewe.

Hupenda kujiendeleza zaidi, katika kujifunza kwa mwanafunzi mtu mzima huwa na malengo ya kufika mbali katika ujifunzaji wake hivyo hupenda kujiendeleza zaidi katika mambo mbali mbali au nyanja mbali mbali.

Mwanafunzi mtu mzima ni mtu ambaye hutegemewa, kwa hiyo katika kujifunza kwa mwanafunzi mtu mzima hakuna uhitaji wa motisha yoyote kwake kwani anakuwa anafanya mambo yake kwa utashi wake mwenyewe na anakuwa na uwezo wa kuongoza watu fulani au hata kutegemewa na watu wengine.

Hupenda maendeleo zaidi kuliko kitu chochote kile, mwanafunzi mtu mzima yeye hupenda maendeleo zaidi anapokuwa katika ujifunzaji wake kwani anakuwa na ufahamu juu ya faida ya kuwa na maendeleo katika maisha ya kila siku.

Kielelezo Na. 18.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 18.

Kielelezo Na. 18.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali. Mtahiniwa alieleza sifa za jumla za mwanafunzi mtu mzima badala ya mambo yanayoweza kufanya mwanafunzi huyo asiwe na motisha ya kujifunza.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA

Kiwango cha ufaulu katika mada zilizotahiniwa mwaka 2020 kilikuwa kizuri kwani asilimia 99.55 ya watahiniwa walipata wastani wa alama 40 na zaidi ambao ni ufaulu wa wastani hadi kuzuri.

Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika mada za mtihani wa 610 Ualimu kinaonesha kuwa watahiniwa walifanya vizuri katika mada saba (7) ambazo ni: *Matayarisho ya Ufundishaji (99.79%), Ufundishaji (99.76%), Makuzi na Ukuaji wa Mtoto (98.25%), Elimu Jumuishi (95.25%), Elimu ya Watu Wazima (94.39%), Saikolojia (94.36%)* na *Nadharia za Kujifunza (73.70%)*. Aidha, mada nyingine tano (5) zilikuwa na ufaulu wa wastani kama ifuatavyo: *Tathmini katika Elimu (69.20%), Upimaji katika Elimu (65.37%), Uongozi wa Elimu Tanzania (61.84%); Maendeleo ya Elimu Tanzania (54.45%) na Ushauri na Unasihi (53.02%).*

Ufaulu mzuri kwenye mada za somo hili unaonesha kuwa watahiniwa wengi walikuwa na ujuzi na weledi wa kutosha kuhusu mada zote zilizotahiniwa katika mtihani wa mwaka 2020.

## 4.0 HITIMISHO

Mtihani wa somo la Ualimu wa mwaka 2020 ulizingatia muhtasari wa somo la Ualimu na ulitahini nyanja zote za utambuzi kama vile maarifa, ufahamu, matumizi, uchambuzi, uundaji na tathmini. Kwa ujumla, kiwango cha ufaulu wa watahiniwa kwa mwaka 2020 kilikuwa kizuri kwa kuwa wastani wa ufaulu wa mada zote ulikuwa ni asilimia 79.98.

Uchambuzi uliofanyika unaonesha changamoto mbalimbali za watahiniwa wachache walioshindwa kupata alama za juu. Changamoto hizo ni kama vile uelewa mdogo wa matakwa ya swali; kutojibu swali zima au kujibu sehemu tu ya swali; kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi; kushindwa kufafanua hoja kwa usahihi na kushindwa kuandika kwa usahihi utangulizi pamoja na hitimisho.

Taarifa hii itasaidia kuendeleza kiwango cha ufaulu katika somo la Ualimu kwani inaweka msingi kwa wakufunzi na wawezeshaji katika ufundishaji wa mada hasa zile zilizoonekana kuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu. Aidha,

taarifa hii itatoa chachu kwa wanachuo na kuwahamasisha katika ujifunzaji wa mada hasa za Upimaji na Tathmini, Uongozi wa Elimu Tanzania, Maendeleo ya Elimu Tanzania pamoja na Ushauri na Unasihi ambazo ni miongoni mwa mada zenye ufaulu wa wastani katika mtihani wa mwaka 2020.

Mwisho, taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa iwe msingi katika kuwasaidia wakufunzi na wanachuo kuyaelewa makosa yanayosababisha watahiniwa wachache kutojibu vizuri maswali na kisha kurekebisha kasoro zilizojitokeza. Aidha, taarifa hii itawasaidia wakufunzi katika ufundishaji, utungaji na usahihishaji wa mitihani yote na hasa ile ya kitaifa hivyo kuinua kiwango cha ufaulu katika somo hili.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Kutokana na taarifa ya uchambuzi wa majibu ya wanafunzi, ufaulu wa wanafunzi ulikuwa mzuri katika mada 7 kati ya 12 zilizotahiniwa. Aidha, mada 5 zilikuwa na ufaulu wa wastani. Ili kuinua kiwango cha ufaulu wa wanachuo katika mada zilizokuwa na ufaulu wa wastani inapendekezwa kuwa:

(a) Wakufunzi na wanachuo wahamasishwe kujisomea makala na machapisho mbalimbali yanayohusu mada za somo la Ualimu hasa katika mada ya Maendeleo ya Elimu Tanzania ili waweze kuendana na mabadiliko mbalimbali yanayotokea kwenye Elimu ikiwemo mabadiliko ya Sera ya Elimu. Hii itawavutia wanachuo wengi kujibu maswali yatakayotungwa kutoka katika mada hii.

(b) Uongozi katika vyuo vya ualimu ujijengee utamaduni wa kualika wageni wenye taaluma ya ushauri na unasihi ili waweze kutoa mhadhara kuhusu mada husika. Mbinu hii itawajengea uwezo wakufunzi pamoja na wanachuo katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada husika hivyo kuinua kiwango cha ufaulu katika mada hii.

(c) Wakufunzi wa somo wajenge tabia ya kutoa mazoezi, majaribio na mitihani ya mara kwa mara ili walimu-wanafunzi wapate uzoefu wa namna tofauti za kuulizwa na kujibu maswali.

(d) Wakufunzi wa somo wawapangie wanachuo katika vikundi vya kujisomea vyenye mchanganyiko wa wanachuo wenye uwezo wa juu na wale wenye uwezo mdogo au wastani. Mchanganyiko huu utasaidia kuinua kiwango cha ufaulu wa wale wenye uwezo mdogo au wastani.

(e) Wakufunzi waandae kwa wingi mazoezi mbalimbali ya ufundishaji kama vile ufundishaji wa somo moja (single lesson), ufundishaji rika na ufundishaji wa kuiga. Mazoezi haya yasisubiri kufanywa wakati walimu tarajali wanapokaribia kwenda kufanya mazoezi ya ufundishaji ya muda mrefu. Hii itawajengea walimu tarajali uwezo zaidi wa kufanya kwa vitendo shughuli zote za ufundishaji, upimaji na tathmini. Mazoezi haya yatawajengea uwezo wa kujibu maswali vizuri katika mada za Tathmini katika Elimu, Upimaji katika Elimu na Uongozi wa Elimu Tanzania.

*Kiambatisho*

**MUHTASARI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA SOMO LA UALIMU**

| Na. | Mada | Na. ya swali | Ufaulu Katika Kila Swali (%) | Wastani wa Ufaulu Katika Kila Mada (%) | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Matayarisho ya Ufundishaji | 5 | 99.79 | 99.79 | Vizuri |
| 2. | Ufundishaji | 13 | 99.76 | 99.76 | Vizuri |
| 3. | Makuzi na Ukuaji wa Mtoto | 12 | 97.08 | 98.25 | Vizuri |
| | | 2 | 99.41 | | |
| 4. | Elimu Jumuishi | 8 | 97.95 | 95.65 | Vizuri |
| | | 10 | 93.36 | | |
| 5. | Elimu ya watu Wazima | 18 | 94.39 | 94.39 | Vizuri |
| 6. | Saikolojia | 1 | 94.36 | 94.36 | Vizuri |
| 7. | Nadharia za kujifunza | 11 | 75.59 | 73.70 | Vizuri |
| | | 4 | 71.81 | | |
| 8. | Tathmini katika Elimu | 7 | 69.20 | 69.20 | Wastani |
| 9. | Upimaji katika Elimu | 15 | 88.01 | 65.37 | Wastani |
| | | 16 | 76.42 | | |
| | | 6 | 31.70 | | |
| 10. | Uongozi wa Elimu Tanzania | 17 | 61.84 | 61.84 | Wastani |
| 11. | Maendeleo ya Elimu Tanzania | 9 | 20.02 | 54.45 | Wastani |
| | | 14 | 88.88 | | |
| 12. | Ushauri na Unasihi | 3 | 53.02 | 53.02 | Wastani |